# Nipashe

Jumatano Oktoba 28, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580382

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



FURSA

Mawakala na wasambazaji wa uuzaji Magazeti

Kwa Maombi na Ufafanuzi zaidi Wasiliana nasi

Meneja Usambazaji na Masoko
Mikocheni Light Industrial Area
S.L.P 31042,
Dar es Salaam,
Tanzania

Namba : +255716500500
Barua Pepe: circulation@guardian.co.tz
Mwisho wa Maombi ni 27 Oktoba 2020

615951602


**42** mbaroni madai vurugu za uchaguzi Pemba, IGP Sirro aonya

UKURASA 3



**TAASISI** za kimataifa zatoa neno uchaguzi mkuu wa Tanzania

UKURASA 4

# UAMUZI




• **Watanzania** milioni 29 kuchagua viongozi leo, wagombea watumia muda wa lala salama kuomba kura... *Endelea ukurasa 2*




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## Maalim Seif Hamad akamatwa, aachiwa

UKURASA 2


**MICHEZO** MENEJA SIMBA ATIMULIWA, KOCHA AOMBA RADHI UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, (IGP) Simon Sirro, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, akiwataka wananchi kudumisha amani wakati wa kupiga kura katika uchaguzi mkuu unaofanyika leo nchini kote. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ni siku ya uamuzi

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

NI siku ya uamuzi! Ndivyo unavyoweza kuiita siku ya leo ambayo imepangwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwa ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Ni siku ambayo Watanzania wanatumia haki yao ya kikatiba kuchagua, Rais, wabunge na madiwani watakaowaongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Katika uchaguzi huo, wagombea 15 wanachuana kuwania nafasi ya Rais wa Tanzania akiwamo Dk. John Magufuli (CCM) anayeomba kuchaguliwa ili aendelee kukalia kiti hicho kwa miaka mitano mingine.

Wagombea katika nafasi hiyo na vyama vyao kwenye mabano ni pamoja na (Benard Membe (ACT-Wazalendo), Twalib Ibrahim (UPDP), Seif Maalim (AAFP), John Shibuda (ADA-TADEA), Queen Sendiga (ADC) na Tundu Lissu (CHADEMA).

Wengine ni Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi), Leopold Mahona (NRA), Hashimu Rungwe (CHAUMMA), Ibrahim Lipumba (CUF), Philipo Fumbo (DP), Khalifa Mohamed Mazarui (UMD), Cecilia Mwanga (Demokrasia Makini) na Mutamwega Migahwya (SAU).

Akihitimisha kampeni zake jijini Dodoma jana, Dk. Magufuli amewataka Watanzania kuendelea kudumisha amani, upendo, mshikamano na kuhakikisha wanawakataa wagombea wanaohubiri vurugu.

Dk. Magufuli pia aliwakumbusha Watanzania kwamba kuna maisha baada ya uchaguzi, hivyo wasiruhusu kuvurugwa wala kuchonganishwa na wagombea wenye maslahi binafsi.

"Kesho (leo) Watanzania watachagua viongozi wao, nipende kutoa rai kwamba kamwe msikubali kuchonganishwa wala kuvurugwa na baadhi ya wagombea, nendeni mkachague viongozi watakaowaletea maendeleo," alisema.

Dk. Magufuli aliwataka Watanzania kuwapuuza wagombea ambao wamekuwa wakihubiri masuala ya kuigawa nchi, kubinafsisha rasilimali za nchi na kufanya vurugu.

Katika mkutano huo, Dk. Magufuli pia aligusia mafanikio katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wake, akisema serikali imedhibiti mauaji ya wazee na vikongwe hususani katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Alisema serikali pia imehamishia makao makuu katika Jiji la Dodoma, mkakati ambao ulikwama kwa miaka 47.

Alisema serikali imefanikiwa kulinda Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao uliasisiwa na viongozi wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Abeid Amani Karume.

"Utawasikia baadhi ya viongozi wanasema wakipewa madaraka, watahakikisha wanauvunja Muungano, ninaomba muwapuuze, kwani Muungano huu umekuwa na manufaa kiuchumi na kijamii," alisema.

Alisema serikali imefanikiwa kujenga hospitali za wilaya 99, kutoka 77 zilizokuwapo tangu nchi inapata uhuru, vituo vya afya 487, hospitali za mikoa 10, hospitali za rufani tatu pamoja na bajeti za dawa kuongezeka kutoka Sh. bilioni 31 hadi Sh. bilioni 270 kwa mwaka.

Alisema serikali pia imefanikiwa kujenga barabara zenye urefu wa kilometa 3,500 na miradi ya maji 1,400 kutekelezwa nchini.

"Tunataka Tanzania ibadilike, tunataka kuionyesha Benki ya Dunia kwamba Tanzania tunaweza, tunataka kuipeleka Tanzania katika uchumi wa kisasa," alisema.

Kuhusu watumishi, Dk. Magufuli alisema serikali imefanikiwa kuwapandisha vyeo watumishi zaidi ya 309,000 na kulipa Sh. trilioni 1.2 za wastaafu.

Alisema wafanyakazi wapya 82,179 wameajiriwa, sekta ya elimu wakiwa zaidi ya 17,000 na afya zaidi ya 14,000.

Dk. Magufuli alihidi kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Jiji la Dodoma ili kutatua kero ya maji katika jiji hilo, akichaguliwa tena kuwa Rais wa nchi.

# Maalim Seif akamatwa, aachiwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, jana alikamatwa na Jeshi la Polisi kisha kuachiwa.

Hata hivyo, Maalim Seif aligoma kutoa maelezo kwa maofisa wa upelelezi baada ya kukamatwa katika kituo cha kupigia kura Garagara, na kuachiwa kwa dhamana ya Sh. milioni 15 ya maandishi.

Akizungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya kuachiwa jana jioni, alisema alikamatwa majira ya saa mbili na nusu asubuhi na Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Mjini Magharibi na kupandishwa katika gari la polisi kuelekea makao makuu ya Jeshi la Polisi, Ziwani Zanzibar.

"Nilipofika nilitakiwa kupanda ghorofa ya mwisho, baada ya kufika niliingizwa katika chumba maalum nikiwa na walinzi wangu wanne, lakini tulikaa muda mrefu bila ya kufahamu kinachoendelea," alisema.

Aidha, alisema kwamba wakati akitafakari kilichotokea, ndipo Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi Zanzibar alipoonana naye majira ya saa 6:00, kisha kukabidhiwa kwa maofisa maalum wa upelelezi ili wamuhoji.

"Niligoma kutoa maelezo bila ya kuwapo wakili wangu na ndipo nilipoanza kumtafuta, lakini mwanzo alipofika alifukuzwa na polisi wakati akifuatilia kukamatwa kwangu," alisema Maalim Seif.

Hata hivyo, alisema baada ya wakili wake kufika aliendelea kusimamia msimamo wake kuwa hayupo tayari kuhojiwa na yupo tayari kutoa maelezo mahakamani.

Baada ya kukamilisha masharti ya dhamana, Maalim Seif alisema polisi walimtaka aende nyumbani kwake, huku akisindikizwa na askari kadhaa na walinzi wake, lakini aliwahoji kwanini wanamzuia kwenda ofisini kwake.

"Waliponifikisha nyumbani waliondoka, na mimi nikatoka na wasaidizi wangu kuelekea ofisini kuzungumza na waandishi wa habari saa 11 jioni," alisema.

Kuhusu uchaguzi mkuu wa leo, alisema ACT-Wazalendo itashiriki kama kawaida licha ya kasoro zilizojitokeza na kuwataka wanachama wake kujitokeza mapema.

Alisema uchaguzi wa kura ya mapema ya jana, umekumbwa na misukosuko ikiwamo watu kadhaa kushikiliwa na Jeshi la Polisi.



# Lissu: Hatima yetu ni mawakala

**Na Elizabeth Zaya**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema hatima ya mwisho ya ushindi wa chama hicho imebaki kwa mawakala wao watakoingia katika vituo vya kupigia kura.

Lissu alisema hayo jana wakati akifunga kampeni za lala salama jana katika viwanja vya Tanganyika Parkers, Kawe jijini Dare es Salaam, kwa ajili ya uchaguzi mkuu unaofanyika leo.

Lissu alisema wao wamefanya kazi ya kuzunguka nchi nzima kwa miezi miwili kunadi sera zao, na wananchi wamewaelewa, lakini hatima ya mwisho imebaki kwa mawakala.

Alisema katika uchaguzi mkuu wa leo, mawakala wao wana kazi ya kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao kwa haki bila kukubali kurubuniwa kwa namna yoyote.

"Sisi tumefanya kazi yetu, lakini tumaini letu kubwa kwa sasa limebaki kwa mawakala wetu," alisema Lissu.

"Tunawategemea mawakala wetu kuikomboa Tanzania, kwa uchache wao, lakini wao ndiyo watakaowakomboa Watanzania walio wengi."

"Tunaomba mtimize wajibu wenu wa kuwa askari wa mstari wa mbele kwa kusimamia na kuwa macho kuliko katika kipindi chochote katika maisha yenu. Tunategemea muwe na msimamo na ujasiri kuliko kipindi chochote katika maisha yenu."

Lissu alisema katika tathmini iliyofanywa na wataalamu wa chama hicho katika kipindi chote cha kampeni, wamebaini kwamba chama hicho kinakubalika kwa asilimia kubwa.

Alisema kila mahali ambapo wamefanya mikutano, ameona matumaini makubwa kwa Watanzania.

"Watanzania wanaamini kesho itakuwa bora kuliko jana na juzi, na haya matumaini lazima tuwapatie majawabu," alisema Lissu.

Mgombea mwenza wa chama hicho, Salum Mwalimu, alisema endapo Watanzania watawachagua, watahakikisha wanamaliza kezo ambazo wamekutana nazo katika siku 60 za kampeni.

Alisema serikali ya chama hicho haitambagua mwananchi yeyoye, na kwamba itahakikisha kila mtu anasikilizwa na kutatuliwa matatizo yake.



Askari Magereza akipiga kura kwenye kituo cha kupigakura cha Miembeni, wakati wa kura ya mapema iliyopigwa Zanzibar jana, kwa ajili ya watendaji wa tume ya uchaguzi na askari wa vyombo vya ulinzi na usalama. **PICHA: ANTHONY SIAME**

# Watu 42 washikiliwa madai kufanya fujo Pemba

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Simon Sirro, amesema wanawashikilia watu 42 visiwani Pemba baada ya kudaiwa kufanya fujo kwa kutupa mawe.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, IGP Sirro alisema katika tukio hilo lililotokea juzi, hakuna mtu aliyefariki dunia.

Aliyasema hayo wakati akizungumzia kuhusu hali ya usalama katika uchaguzi mkuu, unaotarajia kufanyika leo nchini.

"Tumewakamata na sheria itachukua mkondo wake. Ninavionya vikundi vilivyopanga kufanya fujo au vurugu wasijiingize katika uhalifu huo.

"Mkumbuke vijana mnafamilia na wengine mna ndoto zenu, usizikatishe kwa kujiingiza kwenye matatizo, msitumiwe na wanasiasa," alisema.

IGP Sirro aliwataka viongozi wa siasa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), wasimamizi wa uchaguzi na wananchi kwa ujumla, kila mmoja atimize wajibu wake kwa sababu Jeshi la Polisi halitegemei uvunjifu wa amani.

"Tumejipanga vizuri, watakaoleta vurugu tutawashughulikia, mpigakura ukimaliza kupiga kura yako hakuna haja ya kusimama mita 200 eti unalinda, kura yako italindwa na mawakala, ukipiga kura kwa usalama wako rudi nyumbani," alisisitiza.

Vile vile, alisema kauli za baadhi ya viongozi wa siasa kuwatangazia wananchi walinde kura, ni dalili ya kufanya fujo, hivyo wasiifuate.

"Baadhi ya vyama vya siasa vimeona vitandishwa hivyo nia yao ni kufanya fujo. Timu zetu za operesheni na upelelezi zimeanza kazi tangu jana kuhakikisha uchaguzi unamalizika kwa amani na utulivu," alisema.

# ... Wengine 72 watiwa mbaroni Unguja

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WATU 72 wanashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi wakituhumiwa kufanya makosa mbalimbali ya kuchochea uvunjifu wa amani ikiwamo kuchoma matairi barabarani na kuwarushia mawe askari waliokuwa doria.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Awadhi Juma, alisema jana kuwa watu hao wamekamatwa katika maeneo ya Daraja Bovu, Kinuni, Darajani na Mtendeni.

"Tulilazimika kutumia mabomu baada ya kuona viashiria vya uvunjifu wa amani na tunawashikilia watu 72 na watafikishwa mahakamani baada ya uchunguzi kukamilika," alisema.

Kamanda huyo alisema hali ya usalama katika vituo vya upigaji wa kura ya mapema mpaka saa 10:00 jioni ilikuwa ya utulivu na wapigakura walikuwa wanaendelea kujitokeza kabla ya kufungwa kwa vituo.

Pia aliwataka wananchi kutokuwa na hofu kwa kuwa hali ya usalama imeimarishwa kuelekea uchaguzi mkuu unaofanyika leo, huku akiwasihi wananchi baada ya kupiga kura kurejea nyumbani ili kuepusha mikusanyiko isiyo ya lazima.

Hata hivyo alisema katika purukushani hizo hakuna mtu yeyote aliyepoteza maisha, lakini chama cha ACT-Wazalendo kilisema mtu mmoja aliyetambulika kwa jina la Muhammed Juma, amefariki dunia baada ya kupigwa na askari.

"Tuna taarifa ya kwamba Muhammed Juma amepigwa na kufariki (dunia) na tunazo taarifa mwili wake umefikishwa Hospitali ya Mnazi Mmoja," alisema Salum Bimani, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Umma wa chama hicho.

Katika Mji Mkongwe wa Zanzibar, Nipashe ilishuhudia nyumba na maduka yakiwa yamefungwa huku baadhi ya watu wakionekana kuchungulia madirishani na Soko Kuu la Darajani limefungwa.

**"Tuna taarifa ya kwamba Muhammed Juma amepigwa na kufariki (dunia) na tunazo taarifa mwili wake umefikishwa Hospitali ya Mnazi Mmoja," alisema Salum Bimani, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Umma wa chama hicho.**

# Taasisi za kimataifa zatoa neno kuhusu uchaguzi mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI mbalimbali za kimataifa na nchini zimezitaka mamlaka zinazohusika na uchaguzi mkuu, kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na haki.

Aidha, baadhi ya taasisi zimeonya juu ya matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu yaliyoanza kujitokeza.

Katika ukurasa wa Twitter, Balozi wa Marekani nchini, Dk. Donald Wright, aliandika: "Nimeshtushwa na taarifa kutoka Zanzibar na kwingineko za fujo, vifo na watu kukamatwa. Hatujachelewa kuzuia umwagikaji zaidi wa damu."

Aliongeza kuwa: Vyombo vya usalama vijizuie kutumia nguvu kupita kiasi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (ZEC), zitimize wajibu wa uadilifu. Sote tuombe kuwapo kwa uchaguzi wa amani na haki."

Hata hivyo, Mkuu wa Polisi nchini, IGP Simon Sirro, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema hakuna vifo bali watu 42 wamekamatwa kwa kufanya vurugu.

Naye Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Gutierrez, katika taarifa yake iliyotolewa na msemaji wake, Stephane Dajarric, aliwataka wadau wote wa uchaguzi kuhakikisha unakuwa huru na haki.

"Mamlaka zote zinazosimamia mchakato wa uchaguzi mkuu, vyama vya siasa na wagombea wana nafasi ya kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa misingi ya demokrasia na maendeleo endelevu," alisema.

"UN inawataka viongozi wote wa kisiasa na wafuasi wao kushiriki kuhakikisha amani na kukataa vurugu. Tunazitaka mamlaka kutoa ulinzi na kuondoa mazingira ya kuwanyima haki ya kisiasa wananchi," alisema Dajarric.

Katika ukurasa wake, Shirika la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu (UNHR), liliandika: "Tumekuwa tukifuatilia kudumaa kwa demokrasia nchini Tanzania. Tumepokea taarifa za matukio ya watu kuumizwa, kupoteza maisha na kushambuliwa kwa waandishi wa habari, wanasiasa na haki za wanawake kuminywa."



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Stella Ikupa, akifungua mafunzo ya usalama na afya kazini kwa makundi mbalimbali ya watu wenye ulemavu wilayani Rufiji, mkoani Pwani jana. Kushoto ni Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumiaji mtandao watabiri ushindi

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya Watanzania wanaotumia mtandao wa intaneti, wamemtabiria ushindi mgombea wa urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli.

Kwa mujibu wa kura ya maoni iliyofanyika kwa njia ya mtandao (kutayamtandao.com), mpaka jana mchana watu 27,877 walikuwa wamepiga kura na Rais Magufuli ameongoza kwa kupata kura 20, 230 sawa na asilimia 72.57.

Matokeo ya kura hizo yanaonyesha kwamba mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CADEMA), Tundu Lissu, anafuatia kwa kuwa na kura 5,080 sawa na asilimia 18.22.

Uchaguzi mkuu wa mwaka huu ni wa sita tangu Tanzania iliporejea katika mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992. Uchaguzi Mkuu wa kwanza ulikuwa mwaka 1995 na tangu wakati huo, umekuwa ukifanyika kila baada ya miaka mitano kwa mujibu wa Katiba.

Katika uchaguzi wa mwaka huu, wagombea 15 wamejitokeza kuwania urais wakiwamo Magufuli na Lissu ambao ndio wanaoonekana kuchuana vikali kutokana na kampeni walizozifanya maeneo mbalimbali nchini.

Rais Magufuli anagombea urais kwa mara ya pili akiomba achaguliwe tena, ili kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika ngwe yake ya kwanza ya uongozi aliyoianza mwaka 2015.

Katika miaka mitano iliyopita, Rais Magufuli anajivunia kuwapo kwa uboreshaji wa miundombinu ya barabara na reli, maji, elimu na afya, umeme vijijini, ongezeko la makusanyo ya mapato, nidhamu katika utumishi wa umma na matumizi ya serikali.

Lissu kwa upande wake, anajaribu kurusha turufu yake ili achaguliwe huku hoja yake kubwa ikiwa maendeleo, haki na uhuru wa watu.

Katika uchaguzi wa mwaka huu, Watanzania 29,188,347 wamejiandikisha kupiga kura kuamua hatima ya uongozi wa Tanzania kwa miaka mitano ijayo. Uchaguzi huo utafanyika katika vituo vituo 80,155 ambavyo kwa Tanzania Bara ni 79,670 na Zanzibar ni 1,412.

Mtindo wa kura ya maoni kwa njia ya mtandao unakua kwa kasi sehemu nyingi duniani na umekuwa na ushawishi mkubwa katika kuamua ushindi wa mgombea au chama. Wanasayansi wa siasa wanaamini kuwa maoni ya mtandao yenye sampuli ya uwakilishi, hutoa mwelekeo wa picha ya uchaguzi na matokeo ya mchakato huo kwa ujumla.

Takwimu za TCRA zinaonyesha kwamba hadi Juni, mwaka huu, Watanzania wanaotumia intaneti ni 27,100,146.

# Dodoma Mjini mambo ni safi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MSIMAMIZI wa Uchaguzi Jimbo la Dodoma Mjini, Msekeni Mkufya, amesema vifaa vyote kwa ajili ya uchaguzi vimewasili kwa ajili ya kusambazwa kwenye vituo 911 vya jimbo hilo.

Mkufya alisema jana kuwa kutokana na kuwasili huko, tayari vifaa hivyo vimeshasambazwa katika baadhi ya kata.

"Hili jimbo lina kata 41 na jana (juzi) tulisambaza kwa kata 19 na leo (jana) tumemalizia kusambaza kwenye kata 22 zilizokuwa zimebaki. Niwatoe hofu wakazi wa jimbo hili, kuwa vituo vitafunguliwa mapema wajitokeze kwa wingi kupiga kura," alisema.

Pia alisema vifaa vyote viko salama kwenye ofisi za kata na ulinzi utaimarishwa kwenye vituo vyote vya kupigia kura.

"Kuhusu karatasi za kupigia kura zimefika pamoja na zile za nukta nundu. Lakini kama hawataweza kutumia, pia Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imeruhusu kuja na wasaidizi wanaowaamini kwenye vituo ili wawasaidie," alisema.

## Wananchi Kusini Unguja watakiwa kufika kwa wingi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANANCHI wa Mkoa wa Kusini Unguja wametakiwa kujitokeza kwa wingi kupiga kura leo, ili kutimiza haki yao ya kuwachagua viongozi wanaowataka.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Kusini Unguja ambaye ni Mkuu wa Mkoa huo, Ayoub Mohammed Mahmoud, ofisini kwake Tunguu, nje ya mji wa Zanzibar.

Alisema katika kujitokeza kwao kupiga kura ni muhimu kuzingatia sheria za uchaguzi, ili kuhakikisha amani ya mkoa huo inaimarika muda wote.

Mkuu wa Mkoa alisema vyombo vya ulinzi na usalama mkoani humo vimejipanga kuhakikisha amani na utulivu vinaimarika na kwamba watawadhibiti wale wote watakaonyesha viashiria vya uvunjifu wa amani.

Pia aliwataka wafanyabiashara wa vileo nje ya hoteli za kitalii katika mkoa huo, kufanya biashara hiyo hadi saa nne 4:00 usiku.

Aidha, Mkuu huyo wa Mkoa jana, alisitisha shughuli za muziki katika kipindi hiki cha uchaguzi.

HABARI KITAIFA

# Watanzania wapewa neno uchaguzi

Na Christina Mwakangale

KITUO cha Sera za Kimataifa Barani Afrika (CIP), kimetoa wito kwa wapigakura waliojiandikisha kujitokeza kwenye vituo walivyojiandikisha na kupiga kura kwa amani huku wasimamizi wakitakiwa kutokupendelea na kupindisha kanuni na sheria.

Aidha kimesema wapigakura hao wakumbuke kuweka mbele maslahi ya nchi kwa kuchagua viongozi watakaofaa katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa CIP, Omar Mjenga, aliyasema hayo jana akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

"Kuna maisha bada ya uchaguzi, weka maslahi ya nchi yako mbele. Tanzania inapaswa kuendelea kuwa mfano wa kuigwa katika kutunza amani katika kanda ya Afrika na dunia nzima," alisema.

Mjenga alisema pamoja na maandalizi mazuri ya kufanyika uchaguzi mkuu leo, kituo hicho kina matarajio kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) zitahakikisha unakuwa huru na haki kuanzia siku ya upigaji kura na utangazaji matokeo.

"Tunasisitiza kuedelea amani na kufuatwa taratibu zitazosaidia kuwapo uhuru na haki. Tunawaomba kufuata taratibu hizo," alieleza Mjenga.

Alisema kulingana takwimu za NEC, Tanzania Bara kuna wapigakura 29,188,347 na vituo vya kupigia kura 80,155 huku Zanzibar ikiwa na 566,352 ambao walijiandikisha kupiga kura pamoja na vituo 1,413.

Alisema kituo hicho kwa mara ya kwanza kinafanya utazamaji wa uchaguzi mkuu kwa kuwa na watazamaji 93 ambao watapelekwa Zanzibar na katika mikoa 17 ya Tanzania Bara.

Mjenga alisema wito kwa wanaogombea kuanzia nafasi ya urais, ubunge na udiwani pamoja na wadau kuheshimu taratibu na uamuzi wa wapigakura na kwamba siku zote mshindi huwa ni mmoja.

# TAKUKURU yaokoa mil. 33/- za wastaafu

Na Edina Alex, SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Singida imeokoa Sh. milioni 33.5 walizokopeshwa na watumishi wa umma wastaafu na kampuni za kukopesha fedha zenye riba kubwa maarufu kama mikopo umiza bila ya kufuata sheria.

Akitoa taarifa ya utekelezaji huo juzi, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Adili Elinipenda, alisema operesheni hiyo wameifanya kufuatia agizo la Mkuu wa Mkoa huo la kuwatokomeza wakopeshaji haramu ambao wanawakandamiza wananchi hasa watumishi wa umma wanao karibia kustaafu.

"Tumejipanga kikamilifu kuhakikisha hawa wakopeshaji umiza tunawamaliza kabisa ndani ya Mkoa wa Singida na kwa kukuhakikisha leo utawakabidhi wahanga kiasi cha Sh. milioni 33.5 zilizotoka kwa wakopeshaji haramu," alisema Elinipenda.

Alizitaja kampuni ziliyorudisha fedha za wananchi na watumishi wa umma kuwa ni kampuni ya Bomang Microfinance ya Singida mjini ambayo ilimkopesha Mwalimu mstaafu Albert Mpashi, Sh. 7,200,000 na kumtaka arejeshe Sh. 17,000,000 huku Sh. milioni 18,800,000 zimeokolewa kutoka kwa mkopeshaji Biseko Mungeta Kazungu wa Singida mjini, ambaye alimkopesha Mwalimu mstaafu Sh. 2,000,000 na kumtaka arejeshe Sh. 31,000,000.

Wengine ni kampuni ya Magirei Company Ltd (Micro Credit) ya Singida mjini imerejesha fedha za Garase Kajuna, Sh. 17,000,000, huku Widop Company Ltd ikirejesha Sh. 2,400,000 kwa Lucia Nyika, Muuguzi mstaafu, wengine ni Angelva Financial Ltd na Mwita Creditors ya Manyon.

Kwa upande wao waathirika hao Sungi, Kajuna na Nyika walimshukuru Rais Magufuli na uongozi wa serikali yake kwa kuwakumbuka wanyonge kwa kuwa baadhi yao walishapoteza matumaini ya kuishi kama watumishi wastaafu.

"Tunamshukuru Rais wetu Magufuli hakika Mungu ametuletea nabii sio tu rais kwa kuwa kwetu amekuwa baba wa wanyonge, tulipoteza matumaini kabisa, lakini kwa uongozi wake makini tunacheka na kutabasamu," alisema mmoja wa waathirika hao.

Aliwashauri watumishi wengine ambao wapo katika utumishi, kujiandaa vuzuri ili wanapoachana na utumishi wasijiingize kwenye mikopo hiyo.

Akikabidhi fedha hizo kwa waathirika hao, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, aliwapa pole na kuwahakikishia kuwa wakopeshaji haramu ndani ya mkoa huo lazima wabadilike na kufanya kazi zingine huku akiwapongeza watumishi wa TAKUKURU kwa utekelezaji kazi hiyo.

"Mbadilike nyie wakopeshaji umiza, hivi hamuogopi Mungu, alichokopa mtu na anachorejesha mbona haviringani lazima tuwatokomeze, hii sio serikali ya mchezo mchezo," alisema Nchimbi.

Katika hatua nyingine Nchimbi alitoa agizo kwa maofisa utumishi wote ndani ya mkoa huo kuwaangalia watumishi wao ili wasirubuniwe na wakopeshaji hao haramu.

Nchimbi aliutaka uongozi wa mkoa huo kuanzisha dawati lengo likiwa kuwabaini wakopeshaji hao haramu na kuwataka kujisalimisha na wasipofanya hivyo serikali ya mkoa itashughulika nao.


BIASHARA ZOTE MAKINI
HUTANGAZWA HAPA
Nipashe Nipashe mwendo mdundo
Unafahamu ni kwa nini?
"Tunaongoza na Kuaminika"




Nipashe MWANGA WA JAMII
WASILIANA NASI
0745 700 710 au 0677 020 701
advertise@guardian.co.tz (Matangazo)
subscription@guardian.co.tz (Magazeti)
epaper@guardian.co.tz (epaper)
PATA NAKALA YAKO
https://epaper.ippmedia.com
Pakua The Guardian-IPP Media
App Store Google Play
KUWA WA KWANZA KUHABARIKA
TUFUATE nipashetz nipashe TheGuardiantz YouTube TheGuardiantz

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Leo uwe uchaguzi wa kuheshimika duniani*

LEO ndiyo siku ya ukamilishaji wa mchakato muhimu wa kidemokrasia wa kuwachagua viongozi.

Ndiyo ngwe ya wapigakura halali kuwapa haki yao, wagombea waliowavuta na kuwaahidi mambo mengi ili wawapigie kura.

Kwa hiyo wapigakura halali waliojisajili kwenye rejista ya wapigakura ndiyo wanaokwenda kupiga kura kuchagua wabunge, madiwani, wawakilishi, rais wa Tanzania pamoja na wa Zanzibar.

Serikali pamoja na Rais John Magufuli, tangu kuanza mwaka huu waliihakikishia dunia kuwa uchaguzi wa Tanzania utakuwa huru, wa haki, uwazi na unaokubalika.

Ni ahadi iliyotolewa kwa mabalozi wa mataifa mbalimbali kwenye karamu ya kuukaribisha mwaka mpya wa 2020.

Sisi tunawatakia Watanzania kila la heri kwenye uchaguzi huu na kusisitiza kuwa la muhimu ni kuzingatia sheria, kanuni, taratibu za uchaguzi zinazotolewa na vyombo vya kusimamia zoezi hilo.

Kwa wasimamizi hasa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kumbukeni kufanya mambo kwa haki na uwazi ili kuwapa wapigakura viongozi waliowachagua.

Aidha, kwa uwazi na haki, wagombea wavune kile walichopanda baada ya siku 63 za kupiga kampeni zilizoanza Agosti na kuhitimishwa jana.

Tunaamini kuwa kila mpigakura hasa wakongwe wanafahamu kuwa leo siyo wakati wa kampeni, wala kuhamasisha wapigakura kuunga mkono chama chako bali ni siku ya kumchagua kiongozi unayemtaka akuwakilishe kwenye kata, jimbo na kuliongoza taifa.

Kwa hiyo ni ombi letu na kukumbusha kukaa mbali na fulana, mabango ya chama, picha za wagombea, maneno au kauli za kufanya kampeni.

Cha kufanyika leo ni kupiga kura kwa kuweka alama ya tiki kwenye kisanduku kilichoko kwenye jina na picha ya mgombea unayemchagua.

Ni muda wa kuhakikisha kuwa kila mtu anapiga kura bila kuwatenga wengine hasa kinamama ambao wakati mwingine wenza wao huwalazimisha kukaa nyumbani na kutoshiriki kwenye uchaguzi kwa madai kuwa watawachagua wale ambao hawawaungi mkono (chaguo wasilolitaka).

Yapo madai kuwa wanaume au wenza huwanyang'anya wake zao kadi za kupigia kura ili kufanikisha lengo hilo.

Tunawashauri kinamama wasinyamaze wanaponyimwa haki zao hizo. Tunawakumbusha kuwa NEC imewapa wigo mpana wa kutumia kitambulisho cha taifa, leseni na hata pasi za kusafiria ili kuchagua viongozi wanaowataka.

Pengine si jambo jema kukaa kimya ni vyema kueleza mamlaka za kiserikali iwapo mwenza atakukatili na kuchukua kitambulisho ili usipige kura, kwa madai kuwa utakataa chaguo lake.

Aidha, ni wakati wa kuhakikisha kuwa watu wenye mahitaji maalumu kama wazee, wajawazito, wagonjwa na walemavu wanapewa nafasi na kusaidiwa ili kupiga kura zao na asibakie hata mmoja ambaye hakutumia haki yake hiyo kikatiba.

Lengo la uchaguzi ni kuleta maendeleo, hivyo watu wazima wenye miaka 18 na kuendelea wajitokeze kuchagua viongozi wa kuliongoza taifa.

Unapopiga kura hakikisha kuwa unafanya mchakato huo kwa amani na kulinda haki ya kila mmoja ya kuwa salama, furaha na kuendelea na shughuli zake bila bughudha zozote wakati huu wa uchaguzi.

Tuna angalizo, kwa Tanzania tunaona kuwa baada ya miaka karibu 60 ya uhuru ni wakati wa serikali kuangalia uwezekano wa kuruhusu walioko magerezani na hata Watanzania wanaoishi ughaibuni kupiga kura na kuchagua viongozi.


Inaonekana kuwa watu hawa kushirikishwa kupigakura ni jambo linalokuwa la kawaida katika mataifa mbalimbali duniani, hivyo nasi tuwafikirie.

Pengine kazi hiyo inaweza kuwa itahitaji ushirikiano na vyombo vya kusimamia uchaguzi wanapoishi Watanzania hao, lakini cha muhimu ni kuona uwezekano wa kuwashirikisha Watanzania hao.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ubariki uchaguzi mkuu leo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Amani ndiyo maua kuupamba uchaguzi mkuu, kutoa matokeo

Na Sabato Kasika

AMANI, utulivu na mshikamano wakati wote na hata kwenye uchaguzi mkuu ni miongoni mwa mambo muhimu, ambayo wadau wa siasa waliyahimiza na wanaendelea kuyasisitiza.

Waliyasisitiza katika kipindi chote cha siku 63 za kampeni hata leo kwenye sanduku la kupigia kura kwani ni ajenda muhimu kwa kila Mtanzania, kwa kuhakikisha kuwa anailinda wakati wote kwa kutambua kwamba, kuna maisha baada ya uchaguzi.

Amani ni hali ya kutokuwa na vita, mafarakano au chuki na hivyo utulivu, umoja na mshikamano ndivyo vinavyotawala bila kadhia ambazo zinaweza kukwamisha watu kufanya shughuli za kujiletea maendeleo.

Nikirejea kwenye hoja, ni kwamba katika kampeni za uchaguzi mkuu kuliwapo na baadhi ya vitendo, ambavyo vilionekana kuwa, visipodhibitiwa vinaweza kuhatarisha amani, utulivu, umoja na mshikamano miongoni mwa Watanzania.

Hivyo, leo wakati Watanzania wakipiga kura katika uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani, ni vyema kukumbushana umuhimu wa kuepuka vurugu kwa kupiga kura zao kwa usalama na kurudi nyumbani kwa amani.

Kwa maana hiyo, kila Mtanzania atambue na kuzingatia umuhimu wa amani, utulivu, umoja na mshikamano, na kutojihusisha na vitendo ambavyo vinaweza kusababisha tunu hiyo ikatoweka nchini.

Amani, utulivu, umoja na mshikamano viwe ni ajenda ya kila mmoja kuanzia viongozi wa serikali, dini na wanasiasa, wasimamizi wa uchaguzi na wapigakura, kwa lengo la kuendelea kuvienzi kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

Mathalani, hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, alikutana na viongozi na wadau wa siasa na kukubaliana kulinda amani na utulivu kwenye uchaguzi mkuu unaofanyika leo na hata baada ya kuukamilisha.

Katika mkutano huo, Malima anasema, viongozi hao wana wajibu wa kuwaongoza wanachama katika misingi ya sheria ili kuepuka kujihusisha na vitendo vya kuhatarisha amani na utulivu mkoani humo.

Anasema anataka mkoa wake uwe wa mfano kwa kufanya uchaguzi wa amani na salama badala ya kuwa chanzo cha uvunjifu wa amani, na kwamba hilo litawezekana iwapo viongozi na wananchi watashiriki kikamilifu.

Matamanio hayo ya mkuu wa mkoa ni ya Watanzania wote wakiwamo wakuu wa mikoa mingine, vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na raia ili kila hatua hadi kukamilika kwa uchaguzi wa leo, mambo yote yawe salama.

Ni vyema vijana, kwa kuwa ndiyo ambao wamekuwa wakitumika kama mtaji wa baadhi ya wanasiasa kama madaraja ya kuwavusha na hata wakati mwingine kufanya mambo yasiyofaa wasikubali kutumiwa.

Ni vyema wakajitambua na kukataa kutumika kwenye uchaguzi huu, bali wawe wapigakura ama wagombea ili wachague au wachaguliwe na kukataa kushiriki katika fujo za aina yoyote.

Vijana wawe chachu ya kuhamasisha amani kwa kusikiliza maelekezo ya viongozi wa dini, ambayo kimsingi yamejikita zaidi kwenye amani na utulivu ambavyo vimedumu na kuendelea kuwapo miaka mingine mingi.

Kama kuna haja ya kufanya mabadiliko, basi wayafanye kwa kufuata njia halali kuliko zile ambazo zinaweza kusababisha Watanzania waingie katika mtatizo yasiyo ya lazima.

Vilevile ni muhimu vijana kutambua kuwa, wapo baadhi ya wanasiasa, ambao wako tayari kutumia njia zozote kupata madaraka, hivyo wawaepuke ili wasiwaingize mtegoni.

Hivyo leo ambayo ni siku ya kupiga kura, wanasiasa wanaendelea na harakati za kuhimiza amani, utulivu na mshikamano miongoni mwa Watanzania ili wachague rais, wabunge na madiwani bila bughudha.

Wawahimize vijana kujitenga na mambo, ambayo yanaweza kuwaingiza katika matatizo na kuhatarisha umoja na mshikamano wa taifa, kwa kuwa Watanzania ni watu ambao wanaishi kwa pamoja bila kubaguana.

Tanzania yenye amani, utulivu, umoja na mshikamano inawezekana, hivyo ni muhimu hayo yakapewa kipaumbele, kisha masuala mengine baadaye na ikiwezekana yale yasiyofaa yasipewe nafasi.

Vijana ambao ni nguvukazi ya taifa, wawe makini na wanasiasa wenye lengo la kuwatumia vibaya, wawapuuze, ili wasisababishe mgawanyiko miongoni mwa Watanzania, kwa maslahi ya watu binafsi.

Nyufa ambazo zimejitokeza kwenye kampeni na kukomeshwa, zisionekane leo kwenye uchaguzi mkuu, badala yake Watanzania waungane popote walipo kuchagua viongozi wao kwa amani na utulivu.

# EISA watua Tanzania kutathmini uchaguzi

**Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Uchaguzi na Demokrasia Endelevu barani Afrika (EISA), imetua nchini kwa ajili ya kuangalia uchaguzi mkuu unaofanyika leo.

EISA wamefika nchini baada ya kupata kibali kutoka kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kufanya tathmini huru ya mchakato wa uchaguzi.

Ujumbe wa EISA unajumuisha waangalizi 14 waliotoka katika asasi mbalimbali za kiraia na menejimenti za uchaguzi kutoka nchi mbalimbali za Afrika.

Waangalizi hao wametoka Uganda, Afrika Kusini, Zimbabwe, Rwanda na Malawi.

Septemba mwaka huu, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, alisema nchi 15 kupitia balozi zao, zimeruhusiwa kuleta waangalizi wa kimataifa katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Ujumbe huo wa waangalizi wa uchaguzi kutoka EISA unaongozwa na Pansy Tlakula, aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Afrika Kusini na Kaimu Kiongozi wa ujumbe huo ni Grant Masterson.

Hii ni mara ya nne kwa ujumbe wa EISA kuwa waangalizi wa uchaguzi nchini tangu uchaguzi wa mwaka 2000.

Katika uangalizi wao, watajikita kufanya tathmini ya muundo wa sheria zinazosimamia uchaguzi na maazimio ya Umoja wa Ulaya na Umoja wa Afrika yanayosimamia uchaguzi wa kidemokrasia.

Pia, watajikita katika itifaki ya ECOWAS juu ya demokrasia, uchaguzi na utawala na tamko la kimataifa la kanuni za uangalizi wa uchaguzi wa kimataifa.

Waangalizi wa EISA watafanya kazi yao katika mikoa saba ya Tanzania Bara na Zanzibar, ili kuangalia michakato ya awali, kuanzia kampeni, shughuli za kabla ya upigaji kura, siku yenyewe ya kupiga kura na baada ya upigaji kura.

Oktoba 30, ujumbe wa EISA utatoa tamko la ripoti ya tathmini yao ya awali na maoni yao kuhusu mchakato wa uchaguzi, upigaji kura na kuhesabu kura.

Ujumbe huo utaendelea kuwapo nchini hadi Novemba 2 mwaka huu.



Msajili wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Rhoben Nkori (katikati), akizungumza na Msajili Msaidizi wa bodi hiyo, David Jere, katika hafla ya kufunga mafunzo ya siku moja kwa makandarasi wazalendo, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mhandisi Leonard Lucas wa bodi hiyo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali kuwawezesha watu wenye ulemavu

**Na Frank Monyo**

SERIKALI imewahakikishia watu wenye ulemavu kuwa itaendelea kuwawezesha kwa namna mbalimbali ikiwamo kuwapatia elimu ya usalama na afya kazini, ili watoe mchango wao kikamilifu katika maendeleo ya nchi.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu Wenye Ulemavu), Stella Ikupa, aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya usalama na afya yaliyotolewa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa watu wenye ulemavu wilaya ya Rufiji mkoani Pwani.

Ikupa alisema serikali inatambua mchango mkubwa wa watu wenye ulemavu katika maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii, hivyo itaendelea kuliwezesha kundi hilo kwa kuweka mazingira rafiki ya uzalishaji kupitia taasisi zake ikiwamo OSHA.

"Serikali kupitia taasisi kama OSHA na nyinginezo na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), tutaendelea kuwapa mafunzo mbalimbali yakiwamo mafunzo kuhusu masuala ya usalama na afya kazini.

"Pia, tutaendelea kuwawezesha kiuchumi kwa kuwatafutia masoko ya mazao na bidhaa mnazozalisha na kuhakikisha kwamba kunakuwapo na fursa za uwezeshaji ikiwamo upatikanaji wa mitaji," alisema Ikupa.

Akihitimisha hotuba yake ya ufunguzi wa mafunzo hayo, Ikupa aliwaagiza OSHA kuendelea kutoa mafunzo ya kujilinda dhidi ya vihatarishi vya kiusalama na afya katika sehemu za kazi kwa makundi mbalimbali ya watu wenye ulemavu nchini, ili kuwawezesha kufanya kazi katika hali ya afya njema na usalama unaostahili.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya mkakati wa taasisi yake wa kuyafikia makundi mbalimbali katika jamii na kutoa mafunzo ya usalama na afya yatakayowawezesha kufanya shughuli zao kwa kuzingatia kanuni za afya na usalama.

"Hii siyo mara ya kwanza kwa taasisi yetu kutoa mafunzo kama haya kwa watu wenye ulemavu. Tumeshafanya mafunzo hayo katika mikoa mingine ikiwamo Kagera na Dar es Salaam na kwa kuwa ni sehemu ya mkakati wa OSHA.

"Niwahakikishie kwamba mafunzo haya yataendelea kutolewa katika maeneo mbalimbali ya nchi kwa makundi mbalimbali ya watu," alisema Mwenda.

Mshiriki wa mafunzo hayo, Walusimbi Abdul, aliipongeza OSHA kwa kuwapa mafunzo na kutoa wito kwa mamlaka hiyo kuendelea kutoa mafunzo hayo kwa makundi mbalimbali wakiwamo watu wenye ulemavu nchi nzima.

# TAKUKURU yatoa mafunzo uandishi habari uchaguzi

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Ruvuma, imetoa mafunzo ya namna ya kuripoti habari za uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika leo.

Mafunzo hayo ambayo yamefanyika kwenye ukumbi wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma mjini Songea, yametolewa na Mwanasheria wa TAKUKURU, Herman Malima.

Malima alisema waandishi wa habari wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kuwaelimisha wananchi madhara ya kupata viongozi kwa njia ya rushwa na kuwa mfano wa kuigwa katika mapambano dhidi ya rushwa kwa sababu wao ni kioo cha jamii.

Alisisitiza waandishi wa habari wasiandike taarifa ambazo zinaleta uchochezi kwa wanasiasa na jamii kwa sababu kwa kufanya hivyo wataleta machafuko na ukosefu wa amani nchini.

"Sheria ya uchaguzi namba moja ya mwaka 1985 inahusika na kuongoza uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani, inatoa taratibu za uchaguzi na mamlaka mbalimbali ikiwamo kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC). Sheria hii inakemea vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi na inaelekeza adhabu," alikumbusha.

Malima pia alisema viongozi wanaopitishwa kwa njia ya rushwa, hawafai kwa sababu wanasababisha kudumaza uchumi wa taifa kutokana na kuwa watakuwa viongozi wasiopambana na rushwa kwa ukamilifu.

Akizungumza wakati anafungua mafunzo hayo, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma, Hamza Mwenda, alitoa rai kwa wanahabari kuhakikisha wanaripoti habari za uchaguzi kwa weledi na maadili ili kutosababisha machafuko katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu.

Alisema mafunzo hayo yataongeza umakini na uangalifu katika kutafuta, kuchuja na kusambaza habari mbalimbali zitakazokuwa zinaandikwa katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu unaofanyika leo.

**"Sheria ya uchaguzi namba moja ya mwaka 1985 inahusika na kuongoza uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani, inatoa taratibu za uchaguzi na mamlaka mbalimbali ikiwamo kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC). Sheria hii inakemea vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi na inaelekeza adhabu," alikumbusha.**

# Waziri ataka mikopo mitaji kwa wafanyabiashara wadogo

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI za fedha nchini zimeshauriwa kutoa mitaji kwa biashara zinazoanza na kuzisaidia kukua ikiwa ni jitihada za kukuza uchumi nchini.

Ushauri huo ulitolewa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, alipotembelea taasisi za fedha nchini.

Kairuki alizitaka taasisi hizo kuwaunga mkono wawekezaji wanaoanza wakiwa na ubunifu mbalimbali na wenye mawazo mazuri ya biashara††ambao wanakosa mitaji ya kutekeleza mawazo yao.

Alisema watu wenye mawazo mazuri ya ubunifu wanaweza kufanya mambo makubwa iwapo watapewa mitaji na miongozo sahihi kuendeleza ajenda ya serikali kwenye ukuaji wa uchumi.

Kairuki alisema kusaidia biashara zinazoanza ni muhimu kwa ajili ya kukuza uchumi na kutengeneza nafasi††za ajira nchini.

Alisema lazima kuwe na mipango ya kusaidia wawekezaji watarajiwa wa sekta na ngazi zote.

ìTanzania itajengwa na Watanzania hivyo tafuteni namna ya kuwasiaidia mitaji Watanzania wenye mawazo mazuri††ambao wanashindwa kuanzisha biashara kwa sababu tu hawana mitaji ya kufanya hivyo,î alisema.

Waziri aliipongeza benki ya TIB kwa kazi nzuri inayofanya ya kutoa fedha kwaajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa licha ya kwamba ina mtaji mdogo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIB, Charles Singili, alisema benki hiyo inahitaji fedha nyingi ili iwe na uwezo wa kutoa fedha kwaajili ya miradi ya muda mrefu na itemize malengo yake.

ìTunahitaji angalau trilioni moja lakini mtaji wa kuanzia ulikuwa Sh. bilioni 200. Na kufikia Septemba, mwaka huu, benki ilikuwa imewekeza kwenye miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 628.9,î alisema.

Alisema asilimia††75††ya miradi hiyo iko kwenye sekta binafsi na asilimia 25 miradi ya umma wakati asilimia 80 ya miradi hiyo ni ya muda mrefu kuanzia miaka mitano.

Akiwa kwenye benki ya TPB, Waziri Kairuki alisifu ubunifu wa huduma za benki hiyo ikiwemo Songesha ambayo ni huduma ya mkopo kwa njia ya simu inayotoa kwa kushirikiana na kampuni ya mawasiliano inayoongoza.



Mweka Hazina wa Benki ya NMB, Azizi Chacha, akizungumza wakati wa ziara maalum ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, pamoja na ujumbe kutoka Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC) walipotembelea Benki ya NMB kupata uelewa kuhusu mwendo wa sekta ya fedha nchini. Kushoto ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi na Kaimu Ofisa Mkuu wa Fedha, Benedict Baragomwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkumbo aahidi zahanati kupandishwa hadhi

**Na Enock Charles**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Ubungo kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Profesa Kitila Mkumbo, ameahidi kupandishwa hadhi kwa baadhi ya zahanati katika jimbo hilo, kuongezwa kwa zahanati katika baadhi ya mitaa zisaidie kuimarisha huduma za afya jimboni humo.

Akizungumza katika kuhitimisha kampeni zake jana, Profesa Mkumbo alisema kutokana na kuongezeka kwa kasi ya idadi ya watu katika jimbo hilo, ni muhimu kupanua mtandao wa huduma za afya jimboni hapo ili ziendane na kasi ya ongezeko la watu kwa kuboresha hospitali, vituo vya afya na zahanati na kuongeza nyingine zaidi.

"Tunataka tukapandishe hadhi baadhi ya zahanati katika Jimbo la Ubungo, zikiwamo zahanati za Mabibo, Mavurunza na Makurumla ili tuongeze idadi ya vituo vya afya na kupanua huduma za afya katika Jimbo la Ubungo," alisema Profesa Mkumbo.

Alisema akipewa ridhaa katika jimbo hilo atasimamia nidhamu na uwajibikaji kwa wataalamu wa afya, ili watoe huduma kwa wananchi kwa kadri inavyotakiwa na sheria za nchi pamoja na kanuni zilizopo za huduma za afya.

Kuhusu tatizo la ajira Profesa Mkumbo aliwataka vijana na kinamama kuanzisha kampuni za usafi ili kupewa tenda za usafi kutoka manispaa ambazo alisema ni nyingi kutokana na jimbo hilo kuwa na idadi kubwa ya viwanda akitolea mfano wa kata ya Mabibo pekee kuwa na viwanda na maghala yapatayo 16.

Kuhusu kero ya maji katika baadhi ya kata katika jimbo hilo, aliahidi kuwa itakwisha na pia hakutakuwa na usumbufu katika tozo za bili ya maji akijigamba kuwa na uzoefu katika eneo hilo baada ya kupewa nafasi na Rais John Magufuli katika Wizara ya Maji kama Katibu Mkuu wa wizara hiyo kwa kipindi cha miaka mitano.

Kuhusu miundombinu katika jimbo hilo, Profesa Mkumbo alisema atahakikisha barabara katika kata zote nane na mitaa yote 42 ya jimbo hilo inapitika kwa urahisi kwa kujenga barabara zikiwamo za kiwango cha lami na cha changarawe.

# NIT yaanzisha kozi mpya kwa uchumi wa bluu

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuunga mkono juhudi za taifa za kukuza uchumi wa bluu, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimepanga kuanza kutoa kozi za ujenzi na utengenezaji wa meli.

Kozi hiyo maalumu katika kukuza uchumi wa bluu ama 'Blue economy' inatarajiwa kuanza kutolewa chuoni hapo kwa ngazi ya astashahada katika mwaka huu wa masomo wa 2020/21.

Akizungumza na waandishi wa habari katika kampasi kuu ya chuo hicho Mabibo jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Chuo, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema:

"Uchumi wa bluu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa na ustawi wa nchi, ndiyo maana baada ya kuliona hilo chuo kimeamua kuanza kutoa kozi hiyo muhimu kwa mwaka huu wa masomo."

Prof. Mganilwa amesema mbali na kuanzisha programu hiyo, chuo kitaanzisha shahada ya kwanza ya Usimamizi na Usafirishaji katika Bandari (BSPLM).

"Katika mwaka huu wa masomo wa 2020/21, tutaanza kutoa astashahada itakayohusu shughuli za usafirishaji bandarini pamoja na shahada ya mafundi na wahandisi ambao wataweza kujenga meli," alisema.

Alisema vigezo vingine kwa mwanafunzi kujiunga na kozi hiyo, lazima awe amemaliza kidato cha nne na kufaulu angalau masomo manne ukiondoa somo la dini.

Katika astashahada ya ujenzi na ukarabati wa meli, alisema mwanafunzi lazima awe amemaliza kidato cha nne na kufaulu masomo 4 au alama D katika Fizikia/ Uhandisi, Sayansi, Hisabati, Kemia na Kiingereza.

"Ili kusoma kozi hii, mwanafunzi anatakiwa ama awe amemaliza elimu ya ufundi (NVA) kwa kiwango cha level 3 katika nyanja zinazohusiana na uhandisi kama ufundi wa umeme pamoja na ufaulu kwa somo la hisabati kidato cha nne."

Mkuu wa Chuo cha NIT alisema: "Mbali na kuanzisha kozi hizo katika mikakati ya chuo kusaidia kukuza uchumi wa bluu, zitaanzishwa kozi zingine kusaidia mpango huo ikiwamo stashahada ya kawaida katika shughuli za usafirishaji wa barabara na reli pamoja na shahada katika usimamizi na usafirishaji wa barabara na reli (BRRTLM).

**"Uchumi wa bluu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa na ustawi wa nchi, ndiyo maana baada ya kuliona hilo chuo kimeamua kuanza kutoa kozi hiyo muhimu kwa mwaka huu wa masomo."**

# TAKUKURU yaokoa mil. 11/- h/shauri

**Na Jumbe Ismailly,** MKALAMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida imeokoa zaidi ya Sh. milioni 11 zikiwamo Sh. 1,729,000 za makusanyo ya ushuru wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama na kutoingizwa kwenye akaunti ya halmashauri hiyo.

Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Mkalama, Yassin Mohamed Mtaun, aliyasema hayo alipokuwa akimkabidhi Mkuu wa wilaya hiyo, Jackson Masaka, Sh. 11,879,000 kwenye ukumbi wa mikutano wa halmashauri hiyo ili aweze kuzikabidhi fedha hizo kwa wahusika.

Mtaun alifafanua kwamba kati ya kiasi hicho kilichokabidhiwa kwa mkuu wa wilaya huyo, Sh. 1,729,000 ni fedha za makusanyo ya halmashauri, Sh. 150,000 za mwananchi wa Kijiji cha Ishenga na shilingi milioni kumi ni za wachimbaji wa madini wa Kijiji cha Tumuli.

Kwa mujibu wa mkuu huyo, taasisi hiyo pia imeokoa Sh. 150,000 za mwananchi mmoja wa Kijiji cha Ishenga, Rafael Mussa Nsunza, ambazo alidhulumiwa na askari polisi (jina limehifadhiwa), aliyekuwa anafanya kazi kituo cha polisi Ndudguti baada ya kwenda kuripoti polisi tukio la kuibiwa simu yake.

"Rafael Mussa Nsunza mkazi wa Kijiji cha Ishenga alidhulumiwa Sh. 150,000 na askari polisi aliyekuwa anafanyakazi Kituo cha Polisi Nduguti baada ya mwananchi kwenda kuripoti tukio la kuibiwa simu yake na ndipo askari huyo alipomtaka kutoa fedha hiyo kama gharama ya askari huyo kwenda kufuatilia simu hiyo," alisema.

Mtaun alisema TAKUKURU, Wilaya ya Mkalama imeokoa pia Sh. milioni 10 za wachimbaji wadogo kutoka Kijiji cha Tumuli, wilayani Mkalama ambazo ni sehemu ya Sh. 90,000,000 ambazo kampuni ya madini ya Dubu Mining inatakiwa kuwalipa kama kifuta jasho wachimbaji hao wadogo baada ya mwekezaji huyo kuchukua machimbo ya wachimbaji hao.

Vile vile, alisema taasisi hiyo imeokoa magunia mawili na nusu ya mahindi yaliyokuwa yamechangwa na wazazi wenye watoto wanaosoma katika Shule ya Msingi Mkunguru kwa ajili ya chakula kwa wanafunzi wanapokuwa shuleni hapo baada ya viongozi wa kamati ya lishe ya shule hiyo kudai kwamba mahindi hayo yameliwa na wadudu.

# Kiwanda cha zabibu kujengwa Chamwino

**Na Enock Charles**

KIWANDA chenye thamani ya Sh. bilioni 20 cha kuchakata zao la zabibu ili kuzalisha vinywaji mbalimbali kinatarajiwa kujengwa wilayani Chamwino mkoani Dodoma, ili kuwawezesha wakulima kupata tija ya zao hilo.

Akizungumza katika mdahalo kati yake na mgombea mwenzake wa ubunge kupitia CHADEMA uliioratibiwa na chombo kimojawapo cha habari, mgombea ubunge Jimbo la Dodoma Mjini kwa tiketi ya CCM, Anthony Mavunde, alisema kuwa kwa wakulima wa zabibu wamekuwa wakipata hasara ya zao hilo kutokana na kukosa soko la uhakika.

"Tumeanza kuvishawishi viwanda vingi kuja kuwekeza hapa Dodoma kwa ajili ya usindikaji; tuna Mgwabi Holdings, Dani Holdings na hivi sasa anakuja mwekezaji kutoka Arusha anaitwa Kimaro ambaye ndiye anayetengeneza K-Vant anajenga kiwanda chenye thamani ya Sh. bilioni 20 pale Chamwino," Mavunde alisema.

**Mtu kama hawezi kumudu mahitaji yake hawezi kuwa na ufanisi katika kazi yake, mwalimu asipopata maslahi mazuri hawezi kufundisha wanafunzi wake vizuri.**

Mavunde alisema kupitia kuongezeka wa wawekezaji wa zabibu mkoani humo, inatarajiwa kuwa uhitaji wa zao hilo utaongezeka jambo ambalo litasababisha kupanda kwa bei ya zao hilo na kumnufaisha mkulima tofauti na hali ilivyo sasa, ambapo kwa mujibu wa Mavunde wakulima hao wamekuwa wakiuza zabibu yao hadi shilingi 600 kwa kilo ambayo ni bei ya hasara.

Mavunde alijigamba kuwa katika kipindi chake cha miaka mitano kama mbunge, alifanikiwa kukitambulisha kinywaji cha wine ya Dodoma kwa kuanzisha tamasha la wine (wine festival), ambapo wasanii mbalimbali nchini akiwamo Naseeb Abdul almaarufu 'Diamond' alihudhuria tamasha hilo, hivyo kukiongezea thamani kinywaji hicho.

Mgombea kupitia CHADEMA katika jimbo hilo, Aisha Madoga, alisema aliahidi kuboresha maslahi ya wafanyakazi wakiwamo walimu wa shule za msingi na sekondari katika jimbo hilo, ili wafanye kazi kwa ufanisi akieleza kuwa sehemu kubwa ya jimbo hilo inakaliwa na wafanyakazi pamoja na wafanyabiashara.

"Mtu kama hawezi kumudu mahitaji yake hawezi kuwa na ufanisi katika kazi yake, mwalimu asipopata maslahi mazuri hawezi kufundisha wanafunzi wake vizuri," alisema Madoga.

Mgombea huyo pia aliahidi kutatua migogoro ya ardhi aliyodai ni tatizo sugu kwa wananchi wa jimbo hilo baada ya ardhi kudaiwa kugawiwa kwa watu wawili katika eneo moja au mara nyingine ardhi moja kugombewa na taasisi mbalimbali na kundi la watu binafsi.



Mratibu Elimu wa Kata ya Segerea, jijini Dar es Salaam, Hadija Kadia (wa pili kushoto), akimkabidhi cheti mwanafunzi wa Shule ya Msingi ya Kiislam ya Al- Faruku, Annas Binmalik, baada ya kuibuka mshindi wa kwanza katika mitihani ya kumaliza darasa la saba, katika hafla iliyofanyika shuleni hapo, eneo la Tabata juzi. Kushoto ni Mkurugenzi wa shule hiyo, Ali Betiti. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watafiti wapendekeza elimu itolewe kilimo cha mpunga

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATAFITI wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kutoka kwenye utafiti wao wamependekeza Wizara ya Kilimo kupitia sera za kilimo zianze kuhimiza mafunzo ya kilimo shadidi cha mpunga nchi nzima, ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini, hatua itakayosaidia kuboresha maisha ya wakulima.

Mapendekezo hayo yametolewa na Mtafiti Mwandamizi wa masuala ya kilimo na jinsia kutoka kilimo shadidi cha mpunga, Dk. Devotha Kilave, kwenye warsha ya siku moja kwa waandishi wa habari wa vyombo vya habari nchini iliyoandaliwa na mradi wa kutafsiri sera za kilimo barani Afrika (APRA) kwa lengo la kufikisha matokeo ya utafiti wao kwa jamii.

Dk. Kilave alisema kuwa utafiti uliofanyika kuhusu kilimo shadidi cha mpunga umeonyesha wakulima waliopata mafunzo wameongeza uzalishaji kwa kupata mavuno mazuri na kuingia kwenye kilimo biashara na kwamba ni wakati sasa wa sera za kilimo kuhimiza kutoa elimu ya kilimo hicho.

"Kutokana na mafanikio hayo inapaswa Wizara ya Kilimo kutengeneza mkakati wa nchi nzima wa kutoa mafunzo ya kilimo cha mpunga shadidi, ili kuwafanya wakulima kuipenda teknolojia hiyo na kuifanyia kazi ili kuongeza uzalishaji," alisema Dk. Kilave.

Alisema jitihada zozote za kupunguza gharama za uzalishaji na masoko ili kuboresha miundombinu na kupeleka umeme zitasaidia kukifanya kilimo cha mpunga kuwa na faida kubwa kwa jamii.

"Kwenye utafiti wetu tumebaini kuwa mafunzo yana mchango mkubwa sana kwenye kuongeza tija kwenye kilimo, mfano wakulima waliopata mafunzo ya kilimo shadidi cha mpunga wamepata asilimia 8.7 zaidi ya wale ambao hawakupata mafunzo ya kilimo hicho," alifafanua Dk. Kilave.

Alisema kwenye msimu wa kilimo wa mwaka 2016/2017 asilimia 45.8 ya wakulima walianza kilimo hicho, lakini mbinu hiyo baadaye ilisambaa kutoka kwenye vikundi vilivyo pata mafunzo ambao ni asilimia 61.6 na kufikia vikundi vingine 36 ambavyo havikupata mafunzo na vikaanza kilimo hicho.

Dk. Kilave, alisema wakulima wa kilimo shadidi cha mpunga walipata mavuno tani 2.9 kwenye hekta moja wakati ambao hawakutumia mbinu hiyo walipata tani 2.3 kwa hekta moja.

Akizungumzia faida nyingine za kilimo hicho, Mkuu wa Mradi huo, Prof. Aida Isinika, alisema kinasaidia kuokoa upotevu wa maji na uharibifu wa mazingira ikizingatiwa kuwa kilimo hicho cha mpunga kinafanyika jirani na ardhi oevu ya (RAMSA) ambayo inatunzwa.

Kilimo shadidi cha mpunga ni mbinu unayotumia maji na mbegu kwa kufuata kanuni bora za kilimo kama kulima kwa wakati, kupandikiza miche ikiwa na siku siku saba hadi kumi kutoka kwenye kitalu na kupanda kwa nafasi na mistari na kupata mavuno makubwa kuliko cha mazoea.

# Facebook yahakikisha uadilifu kuelekea uchaguzi mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

MTANDAO wa Facebook umesema kuwa utahakikisha uadilifu unakuwapo katika maudhui inayorushwa mtandaoni, ili kulinda demokrasia kwenye uchaguzi mkuu nchini.

Aidha, mtandao huo umezindua njia zitakazotumika kuzuia kuenea kwa upotoshaji wa maudhui ya siasa au uingiliaji wa masuala ya uchaguzi mkuu.

Mkuu wa Sera za Jamii wa Facebook kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika, Mercy Ndegwa, aliyasema hayo hivi karibuni katika mjadala wa waandishi wa habari juu ya shughuli zinazofanywa na mtandao huo.

Alisema kuwa mtandao huo unafanikisha ushiriki wa kiasiasa, kama njia ya kujenga jamii yenye uelewa na ushiriki sahihi katika masuala ya kisiasa kuelekea uchaguzi mkuu na kwamba watazindua ujumbe maalum kuwakumbusha Watanzania siku ya kupiga kura.

**Habari hiyo inazuiliwa kusambaa kwake ili kuizuia habari hiyo isiendelee kupotosha jamii na wakati huo huo habari sahihi zinazoendana na habari husika itakayotajwa kupotosha zitatafutwa na kupostiwa ili kuifafanua.**

Alisema kutakuwa na taarifa muhimu za upigaji kura zitakazokuwa shirikishi kwa watumiaji wa Facebook kwa kuwa unawaruhusu kuusambaza ujumbe huo kwenye kurasa zao za mitandao ya kijamii kwa njia ya picha na watasambaza picha kuonyesha furaha ya upigaji kura hatua itakayohamasisha ushiriki wa Watanzania wengine kwenye uchaguzi mkuu.

Ndegwa alisema katika kukabiliana na upotoshaji wakati wa uchaguzi mtandao huo, itafuatilia taarifa kwa kuangalia ufanisi wa taarifa zinazotumwa kwenye kurasa za Facebook na Instagram na watakaorusha ujumbe usiofaa hatua zitachukuliwa.

"Habari hiyo inazuiliwa kusambaa kwake ili kuizuia habari hiyo isiendelee kupotosha jamii na wakati huo huo habari sahihi zinazoendana na habari husika itakayotajwa kupotosha zitatafutwa na kupostiwa ili kuifafanua," alisema.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, wataongeza uwazi kwenye matangazo ya kisiasa na kwamba kila anayetaka kutoa tangazo la siasa anapaswa kuthibitishwa kuwa wao ni kina nani na kama wanaishi Tanzania.

Katika kuhakikisha usalama wa wananchi, wanawahakikishia matumizi salama ya mitandao, kipaumbele kikubwa kwetu hasa wakati wa uchaguzi mkuu, na kwamba kidunia, Facebook imeongeza idadi ya watu wanaoshughulikia usalama wa matumizi ya mtandao wake kufikia hadi 35,000 ikijumuishwa na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.

"Tunafurahia kazi zetu Tanzania. Kama kampuni tumewekeza pakubwa kuhakikisha kwamba Facebook ni sehemu watu wanajiskia salama, wanapata taarifa sahihi na sauti zao zinasikika. Tunaamini kwamba kazi tunayoifanya kuhakikisha uadilifu wa uchaguzi Tanzania itasaidia kupunguza usambazaji wa habari potofu, kuzuia uingiliaji wa uchaguzi na kukuza ushiriki wa raia," alisenda Ndegwa.



Wafanyabiashara wa samaki aina ya pweza, dagaa kamba na aina nyinginewakiwaandaa kwa ajili ya kuwauzia wateja katika eneo la Mwananyamala Mwinjuma Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# RC awaomba viongozi dini uchaguzi mkuu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ametoa rai kwa viongozi wa dini kuwashirikisha waumini wao kwenye nyumba za ibada kuliombea taifa kuelekea uchaguzi mkuu wa leo, ili ufanyike kwa utulivu na amani.

Ndikilo alitoa rai hiyo katika kikao cha kamati ya amani ya mkoa huo, mjini Kibaha. Alisema mkoa huo umekamilisha maandalizi yote kwa ajili ya kupiga kura, na yote hayo hayawezi kufanyika bila huruma ya Mungu.

Mkuu huyo wa Mkoa alisema ni jukumu la viongozi wa dini kuzidisha maombi kuomba amani, ili kura zipigwe kwa amani na utulivu na mshindi atangazwe bila shinikizo.

Alisema serikali itahakikisha uchaguzi unafanyika kwa amani na utulivu, na kwamba mkoa huo unatarajia baada ya kupiga kura zihesabiwe kwa utulivu na mshindi kutangazwa bila kikwazo ili mkoa huo uendelee kubaki na hali ya amani baada ya uchaguzi.

Aliwasisitiza wananchi wenye sifa kujitokeza kupiga kura kutimiza wajibu wao na kuzingatia kikamilifu maelekezo kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Mwenyekiti Mwenza wa Kamati ya Amani ya Mkoa wa Pwani, Hamis Mtupa, alisema kipindi chote cha kampeni hapakuwa na uvunjifu wa amani, hivyo kuwaomba wananchi kuendeleza amani siku ya uchaguzi leo.

Alisisitiza wananchi kurudi nyumbani baada ya kupiga kura, huku akitoa tahadhari kwa Jeshi la Polisi kuhusiana na mkesha wa Maulidi ambao utakuwa siku ya kupiga kura.

Naye Padri Benno Kikudo, alisema wanaendelea na maombi kuiombea nchi kufanya uchaguzi kwa amani, huku akiwasihi wagombea kuwa tayari kupokea matokeo baada ya kura kupigwa.

Ahmad Seif, mmoja wa wajumbe wa kamati ya amani, aliiomba serikali kuwezesha kamati hiyo ya mkoa kufika maeneo ya shule kuwaelimisha vijana umuhimu wa kulinda amani.

Seif alisema serikali inatakiwa kuangalia namna ya kutengeneza amani kuanzia shuleni kwani kundi la vijana ndio linalochangia kupotea kwa amani.

# Ongezeko la faida NMB lapaa

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya NMB imepata ongezeko la asilimia 76 la faida kabla ya kodi kwa kipindi kilichoishia Septemba 30, mwaka huu.

Akitangaza matokeo ya robo ya tatu ya mwaka 2020 ya benki hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Ruth Zaipuna, alisema matokeo hayo yamesababishwa na kukua kwa haraka kwa uchumi wa Tanzania, sera wezeshi na mwendelezo wa ukuaji wa pato la taifa kwa miaka ya hivi karibuni.

Zaipuna alisema pia utendaji mzuri wa kifedha wa benki hiyo kwa mwaka huu, ubora wa wafanyakazi na imani ya wateja kuendelea kutumia huduma zao zimechangia mafanikio hayo.

"Kwa miaka mitano sasa, Tanzania imeshuhudia ukuaji imara wa uchumi uliowezeshwa na sera thabiti za kiuchumi za serikali ya awamu ya tano. Maendeleo haya, mazingira rafiki ya kibiashara, pamoja na utekelezaji mzuri wa mikakati ya benki yetu ni sababu kuu za ongezeko hili la faida katika robo ya tatu ya mwaka 2020," alisema Zaipuna.

"Katika kipindi hiki faida kabla ya kodi ya Benki ya NMB imepanda kwa asilimia 76 kutoka Sh. bilioni 118 katika robo ya tatu ya mwaka 2019 hadi Sh. bilioni 208 mwaka huu, wakati faida baada ya kodi imepanda kutoka Sh. bilioni 82 hadi Sh. bilioni 145 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 77.

Zaipuna alisema katika kipindi hiki, mkakati wa Benki ya NMB wa kukuza vyanzo vya mapato umejidhihirisha kwa ongezeko la mapato yatokanayo na uendeshaji kwa asilimia 14 kutoka Sh. bilioni 527 katika robo ya tatu mwaka 2019 hadi Sh. bilioni 600 katika robo ya tatu ya mwaka huu.

Zaipuna alisema katika kipindi hiki, programu za benki hiyo za kudhibiti gharama za uendeshaji na matumizi ziliimarishwa na kusababisha uwiano mzuri wa gharama na mapato kwa asilimia 52.

"Benki ya NMB kama mwezeshaji mkubwa wa maendeleo na uchumi nchini, imekuza rasilimali zake kwa asilimia 15, kutoka Sh. trilioni 6.1 kipindi kama hiki mwaka jana hadi Sh. trilioni 7 katika robo ya tatu ya mwaka 2020 na imesababishwa na ongezeko la amana za wateja kwa asilimia 15 na ongezeko la mikopo kwa wateja la asilimia 16.

Pia alisema eneo jingine ambalo benki hiyo imepata mafanikio ni katika ukopeshaji kwa kupunguza lengo la mikopo chechefu kwa asilimia 22 ukilinganisha na kipindi hicho kwa mwaka 2019.

## Baada ya siku 63 za kampeni...

Ukurasa 12





Ukurasa 13

## Mazoea yalipobadilishwa kusikiliza kuliko kuhutubia

**siasa**

JUMATANO OKTOBA 28, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

### LEO NDIYO SIKU YA JAMBO LETU

# Usisahau wajibu wako kuleta uchaguzi ulio huru, wazi, haki

**Na Mwandishi Wetu**

UCHAGUZI Mkuu ni mchakato wa kuchagua viongozi watakaowawakilisha wananchi kwenye ngazi mbalimbali za uwakilishi kuanzia bunge, udiwani na urais ambayo ni mamlaka ya juu kwenye uongozi.

Mara nyingi kwenye uchaguzi huibuka misemo ya kuhamasisha wapigakura, mwaka 2015 hamasa kama 'toroka uje' zilitumiwa kuwachagiza wananchi kushiriki kwenye kampeni na kupiga kura.

Uchaguzi Mkuu wa 2020 kibwagizo cha 'tuna jambo letu' ndicho kinachotawala anga la Tanzania kuhamasisha umma kujitokeza kupigakura.

Wakati wa sherehe za kuukaribisha mwaka 2020, Rais John Magufuli, alipokutana na mabalozi wa mataifa mbalimbali jijini Dar es Salaam, aliwaahidi kuwa uchaguzi utakuwa wa huru na haki na hilo ndilo Watanzania wanaloliamini.

Wakati Watanzania wanapoelekea kwenye sanduku la kura asubuhi hii wanapenda kuushuhudiwa uchaguzi ulio uhuru, wa haki na matokeo yake yanayokubalika na wadau wote.

Leo ndiyo Jumatano Oktoba 28, siku ya kupiga kura, cha kwanza watu wafahamu ili uwe mpigakura ni lazima uwe Mtanzania, ufikie miaka 18, uwe mkazi unayefahamika na uongozi wa serikali za mitaa unakopigia kura na la muhimu uwe umejiandikisha na kujihakiki kwenye daftari la kudumu la wapigakura. Wewe ni halali kapige kura yako.

Kwa hiyo hatua ya kwanza ya kuufanya uwe huru na wa haki inaanza na wapigakura wanaoelekea kwenye vituo vya uchaguzi leo, wawe wamesajiliwa kwenye daftari au rejista ya kudumu ya wapigakura.

Ili uwe na sifa hizo na matokeo ya uchaguzi yakubalike na wadau



Vifaa vya kupigia kura , wasimamizi kuwahi vituoni na kufanyakazi kwa uwazi pamoja na ulinzi na usalama ni miongoni mwa mambo yanayohitajika leo uchaguzi mkuu unapofanyika nchi nzima. **PICHA: MTANDAO.**

hasa wapigakura na wanasiasa waliogombea ni lazima wahusika wakuu na wasimamizi ikiwamo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), wawajibike na kutenda kila jambo kwa haki na uwazi.

Jambo jingine linaloufanya uwe wa haki ni vyombo vya kusimamia uchaguzi, asasi za kiraia, vyama vya siasa, tasnia ya habari na wanasiasa viwe vimeshiriki kikamilifu kuueleza umma na wapigakura uzuri wa kushiriki kwenye jukumu la kuchagua viongozi ili watu wengi wajitokeze kupiga kura.

Ndiyo elimu ya uraia, na kwamba haki inasimama pale taasisi na vyombo vya usimamizi vitakapofanyakazi kwa maadili na uwazi bila woga, hofu wala upendeleo.

**VYOMBO VYA HABARI**

Ili kura zinazopigwa leo zilete uchaguzi ulio huru na haki vyombo vya habari ambalo ni daraja muhimili kuanzia sasa viruhusiwe kutoa taarifa na mwenendo mzima wa uchaguzi bila kukwazwa.

Viwe huru kuelezea mchakato huo kwa kusikiliza maoni ya wananchi, vyama vya siasa na wagombea na kuwafikishia wananchi taarifa sahihi na za zilizo na ulinganifu na zisizoleta hisia za chuki.

Asasi za kiraia ambao ni sehemu ya waangalizi wa ndani pamoja na wale wa kimataifa waruhusiwe kufanya jukumu lao kwa uhuru na haki.

Vyombo vya usimamizi wa uchaguzi viwajibike kwa kuhakikisha wasimamizi vituoni wanawahi na kuvifungua mapema iwezekanavyo.

Vifaa vya uchaguzi ikiwamo rejista ya wapigakura kwa kila kituo iwe imefikishwa ili kufanikisha uhakiki na upigaji kura unafanyika bila vipingamizi.

Vitu vingine kama karatasi za majina ya wagombea, wino, muhuri na peni viwahi kwenye vituo na siyo kuletwa baadaye ili kuepusha kuchelewa kupigakura au kuendelea hadi siku ijayo.

Usalama ni jambo la muhimu hivyo NEC ihakikishe uwepo wa usalama wa kutosha vituoni, lakini siyo wa kuwatishia wananchi maana wakati mwingine kinaweza kuwa chanzo cha watu kuvikimbia vituo vya kura.

**MATOKEO KUCHELEWA**

Mara nyingi kumekuwa na matatizo ya kukawia kutoa matokeo, hili liepukwe matokeo yatangazwe haraka ili kuondoa sintofahamu na lawama zinazohusishwa na wizi wa kura.

Wakati matokeo yakitangazwa walioshindwa wawe huru kupinga matokeo mahakamani kwa mujibu wa sheria na taratibu haraka iwezekanavyo.

Kupiga kura ni haki japo ni mchakato wenye gharama, hakuna sababu ya kuharibu karatasi la kura. Kinachohitajika ni kuweka tiki kwenye kisanduku kilicho mbele ya jina na picha ya mgombea, hilo pekee ndilo la kufanya.

Kwenye karatasi ya kura hakuna sababu ya kuchora, kuandika au kutukana wagombea kufanya hivyo ni kuiharibu kura yako. Cha muhimu ni kuweka tiki kwenye kisanduku kilichoko mbele ya watu unaowachagua, kwa rais na mgombea mwenza.

Kadhalika, kwenye ubunge unaweka tiki kwenye kisanduku kilicho mbele ya picha yake na vile vile kwa diwani wako.

Baada ya kupiga kura kunja karatasi kwa marefu mara moja na itumbukize kwenye sanduku la kura, hakuna kingine zaidi ya hapo ni kurudi nyumba au kuendelea na shughuli zako ukisubiri matokeo.

# Baada ya siku 63 za kampeni...

## •Leo kila mgombea kuvuna alichopanda

**Na Sabato Kasika**

ZAIDI ya Watanzania milioni 29 waliojiandikisha kupigakura leo wanawachagua viongozi kwenye uchaguzi mkuu wa sita ndani ya mfumo vyama vingi vya siasa.

Mwaka huu idadi ya wapigakura imeongezeka zaidi ikilinganishwa na ile ilioandikishwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, ambayo ilikuwa ni milioni 23.1, hali inayoonyesha kuwa kumekuwapo na mwamko zaidi.

Idadi hiyo ya wapigakura ilitangazwa hivi karibuni na Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufaa, Semistocles Kaijage, ikiwa ni ongezeko la asilimia 26 ya wapiga kura wapya.

Mwenyekiti huyo anasema hao ndiyo ambao watapiga kura kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu katika vituo takribani 80,155, na kwamba kila kituo kitakuwa na wapigakura wasiozidi 500.

Leo ni siku ya kupiga kura baada ya kampeni za siku 63 zilizoanza Agosti 26 na kumalizika jana, zikiwapa nafasi wagombea urais, ubunge na udiwani wa vyama mbalimbali vya siasa kunadi ilani na sera za vyama vyao.

Zaidi ya vyama 10 vimeweka waagombea urais katika uchaguzi huo unaofanyika leo, kikiwamo Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC) kinachowakilishwa na Queen Sendinga.

Vyama vingine ni cha Demokrasia Makini, mgombea wake ni Cecilia Mwanga, CCM Rais John Magufuli na CHADEMA ni Tundu Lissu.

Katika mlolongo huo, kipo Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, Sauti ya Umma (SAU), mgombea ni Muttamwega Mgaywa na NCCR- Mageuzi kinachowakilishwa na Jeremiah Maganja.

**SINTOFAHAMU ZILIZOIBUKA**

Katika hatua za mwanzo za kupendekeza na kuwasilisha majina ya wagombea urais, ubunge na udiwani, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea rufaa 557 kutoka kwa wagombea kuhusu uteuzi wa wagombea wa nafasi hizo katika uchaguzi mkuu unaofanyika leo.

Rufaa hizo zinatokana na baadhi ya wagombea ubunge na udiwani kutoridhika na maamuzi ya wasimamizi wa uchaguzi na kwamba baada ya kupokea rufaa ilianza kuzifanyika kazi na kuzitolea uamuzi mapema.

Ndivyo Mwenyekiti wa NEC Jaji Kaijage alivyowahi kukaririwa na vyombo vya habari akisema, jijini Dar es Salaam, kutokana na malalamiko ya baadhi ya wagombea.

Hali hiyo ilitokana na baadhi ya wagombea ubunge na udiwani kulalamikia wakurugenzi wa halmashauri kwamba waliwaengua ama kukataa kupokea fomu zao bila sababu za msingi.

Si hilo tu, bali pia kulikuwa na malalamiko kwamba, baadhi ya wakurugenzi wao walifunga ofisi na kusababisha wagombea kushindwa kurejesha fomu zao za uteuzi kwa wakati na hivyo kukosa sifa.= Hali hiyo ilisababisha NEC kuingilia kati na kuwarejea baadhi ya wagombea kwenye kinyang'anyiro, lakini pia kukiwa na majimbo na kata, ambazo wagombea walipita bila kupingwa.



Mgombea urais kwa tiketi ya ADC Queen Sendiga, akifanya kampeni mitaani . **PICHA: MTANDAO.**

**MAWAKALA KUTOAPISHWA**

Ndani ya sintofahamu hiyo, hatimaye kampeni za uchaguzi zilianza na sasa zimehitimishwa lakini pia kukiwa na malalamiko mengine ambayo ni ya mawakala wa baadhi ya vyama kudai kutoapishwa.

CHADEMA ni miongoni mwa vyama vinavyolalamikia 'figisu' katika kuapishwa kwa mawakala wa vyama vya siasa watakaosimamia uchaguzi mkuu katika maeneo mbalimbali nchini.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari, Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika anadai kwamba, baadhi ya mawakala hawapewi ushahidi wa nakala ya barua za kuapishwa.

Mnyika anaamini kwamba, hali hiyo itasababishwa wakataliwe kuingia katika vituo vya kupigia kura, kwa kigezo cha kutotambuliwa kwenye vituo husika, hivyo ni mihumu tatizo hilo likatatuliwa mapema. Kwa upande wa NEC, iliongeza siku tatu za kuapishwa kwa mawakala kwa vile baadhi ya maeneo yana tatizo la kutofikika kirahisi, kutokana na jiografia hali iliyosababisha wasimamizi kutowafikia maeneo husika kwa wakati.

**KUOMBA KURA KIAINA**

Kampeni hizo zilizohitimishwa jana, zilijaa vimbwanga vya aina mbalimbali, ikiwamo wanasiasa kurushiana vijembe, kebehi na baadhi yao kuwapigia magoti wananchi wakiwaomba wawachague.

Wapo waliofikia kulala chini katika mikutano ya kampeni na kuomba kura, huku wengine wakitembea kwa magoti kuonyesha heshima kwa wapigakura ikiwa ni moja ya mbinu kutafuta kura.

Katika mbinu hizo za kutafuta kura, baadhi ya wagombea ama wapambe wao walikuwa wakiwaita wapinzani wao majina ya kudhalilisha ili wananchi wawadharau na kuachana nao.

Pamoja na hayo na mengine mengi, jambo kubwa ambalo wanasiasa walikuwa wakihimizwa na wadau wa siasa wakati wote kulinda amani, utulivu na mshikamano uliopo nchini, wakati wa kampeni na baada ya uchaguzi.

Miongoni mwa wadau hao ni Waziri Mkuu Mstaafu John Malecela, ambaye akiwa nyumbani kwake jijini Dodoma anajitokeza kuuasa umma wa Watanzania kuepuka wanasiasa wenye nia ya kuvuruga amani.

Anasema, Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, ameiacha nchi katika misingi ya umoja na amani, hivyo ni muhimu kuendeleza hali hiyo kwa maslahi ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

"Uchochezi na ubaguzi kwa misingi ya udini na ukabila ni mambo ya kukemea kwani vinaweza kusababisha mpasuko katika makundi ya jamii na wakati mwingine hata machafuko," anasema Malecela.

Anawataka Watanzania kupuuza kauli za uchochezi na hakuna watu wanaoweza kuwalazimisha kumchagua mgombea kwa msingi wa dini yake bali, waangalie vigezo, ambavyo wanavipenda ikiwamo maendeleo na umoja wa kitaifa na kuacha kujadili vitu visivyokuwa na manufaa kwa nchi.



Boniface Jacob, mgombea ubunge wa CHADEMA jimbo la Ubungo (mwenye kofia nyekundu) ni miongoni mwa wagombea waliowasilisha rufani NEC kupinga kuenguliwa, Tume ya Uchaguzi ilimrudisha kwenye nafasi hiyo. **PICHA: MTANDAO.**

# Mazoea yalipobadilishwa kusikiliza kuliko kuhutubia



Mgombea urais Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, katika kampeni za uchaguzi mwaka huu. Aidha, alitumia fursa hiyo kukutana na makundi mbalimbali kusikiliza maoni yao badala ya kuwahutubia. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPENI za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 zimemalizika na leo kazi ni moja kupiga kura na kusubiri matokeo yatakapotangazwa wakati wowote baada ya kazi hiyo kukamilika.

Ni hatua kubwa kwenye suala la kuienzi na kuiendeleza demokrasia ambayo inawapa Watanzania uhuru wa kuchagua viongozi watakaowaongoza kwa miaka mitano.

Katika hekaheka za kutafuta kura na kuwavutia wananchi kwenye kampeni kuna mambo kadhaa yaliyojitokeza mengine ikiwa ni mara ya kwanza mathalani mgombea urais wa CCM visiwani Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuwasikiliza badala ya kuwahutubia wapigakura.

Hatua, hiyo ni mkakati wa kipekee ambao mgombea huyo alitumia kukutana na kuzungumza na makundi mbalimbali ya wafanyakazi, wajane na wafanyabiashara.

Katika kampeni hizo Dk. Mwinyi aliozungumza nao ni pamoja chama cha walimu Zanzibar, jumuiya ya wawekezaji, sekta ya utalii, ushirika wa vyama vya wafanyakazi, wavuvi, wafugaji, wakulima, viongozi wa dini, wajasiriamali, jumuiya ya wajane na Wazanzibari wanaoishi ughaibuni diaspora.

Baadhi ya maoni yanayotolewa na wanajumuiya ya wajane Zanzibar, yanamshawishi Mwinyi kuahidi kusimamia haki zao na kutunga sheria za kulinda maslahi yao na kwamba itafanikisha kuwabana baadhi ya wanaume wanaotelekeza watoto wanapowaacha wanawake.

Baadhi ya mambo yanayobainishwa kuwa yanawakwaza wajane ni kukoseshwa haki zao, kuporwa mali na kufukuzwa kwenye nyumba huku na mateso mengine na udhalilishaji dhidi yao.

Wanajumuiya ya Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi anasema wapo Wazanzibari wanaoishi nchi mbalimbali kama Denmark ,Oman, Uingereza Ethiopia, China na Canada wanaoeleza changamoto kama kunyimwa vibali vya kumiliki ardhi kwa kisingizio kuwa si wazawa na hata kukanwa na masheha maeneo wanakotoka.

Chama cha Walimu wanamweleza mgombea kuiangalia tena sekta ya elimu na kuwajali walimu ambao ni muhimu wanaozalisha viongozi bora, wasomi na wanahusika na kila eneo la maendeleo ya nchi.

Akizungumzia hatua hiyo ya kuwasikiliza wananchi badala ya kuwahutubia, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, anasema ni mkakati wenye ongezeko la thamani kwa kuwa unampa mgombea nafasi ya kuwasikiliza watu waseme wanachotaka badala ya kuwaeleza kile anachodhani ndicho wanachotaka awafanyie.

Anapozungumza na Nipashe, aidha anasema ni mbinu bora ya kampeni ambayo inawasogeza karibu zaidi wagombea na wapigakura wao na kuongeza uhuru wa kutoa mawazo na maoni na kusikilizwa.

"Inawezekana katika kampeni mgombea anapanga vipaumbele anavyohisi vinavutia kuwapelekea wananchi lakini wao wakaona kuna jambo jingine hivyo katika mijadala hiyo ni fursa ya kufahamu zaidi maoni ya wapigakura."

> "Inawezekana katika kampeni mgombea anapanga vipaumbele anavyohisi vinavutia kuwapelekea wananchi lakini wao wakaona kuna jambo jingine hivyo katika mijadala hiyo ni fursa ya kufahamu zaidi maoni ya wapigakura."

Mkurugenzi wa LHRC anasema mkakati huo unaongeza wigo wa demokrasia kwa vile unawapa wananchi fursa pana zaidi ya kutoa maoni yao, kukosoa serikali na kuelekeza namna bora ya kuwajibika zaidi.

Anasema mara nyingi katika kampeni imekuwa ni mazoea kusikiliza wagombea zaidi , lakini utaratibu wa Dk. Mwinyi umewapa wapigakura haki ya kutoa maoni, kusikilizwa, kukosoa serikali na tasisi zake pamoja na kuishauri.

Anakumbusha kuwa hiyo ni njia ya kuifanya serikali yake iwapo itachaguliwa kuongoza kwa miaka mitano, kuwajibika kwa makundi mbalimbali na kukumbushwa kile mgombea alichowaahidi wapigakura kwenye vikao vya ndani, aliposikiliza maoni ya makundi mbalimbali.

Aidha, anashauri kupanua wigo na kuyafikia makundi yenye uhitaji kama walemavu (bubu) wasioweza kuongea, viziwi bubu wasiosikia wala kuzungumza ambao wanahitaji kuwapo watu wa kuzungumza lugha ya alama.

Anasema wanahitaji kwenye vituo vya polisi, mahakamani, hospitali na kwenye kampeni za siasa ili watoe maoni yao, wakosoe na kueleza kile wanachoona kinawakwamisha au kikifanyika kitaboresha maisha yao.

Henga anadhani ni muhimu pia wakati huu wa kupiga kura na kutangaza matokeo kuwe na wanaotafsiri na kuzungumza lugha ya alama ili wahitaji hao wawe sehemu ya mchakato.

Kwa upande mwingine , Gladness Munuo, Mratibu wa Kituo cha Utatuzi wa Migogoro (CRC) , anasema wakati wa kampeni kila mmoja anaweza kubuni mbinu yake ya kufikia wapigakura lakini pamoja na vikao vya ndani vya kukutanisha wadau na makundi mbalimbali, wananchi wameruhusiwa kutumia simu na kuwafikishia ujumbe wagombea.

Munuo anaeleza kuwa ni fursa kuwapa maoni yao, kero na changamoto zao , kukosoa na kupendekeza mambo wanayotaka mgombea ubunge, urais na hata udiwani kuwatimizia.

"Hii inawezekana kupitia twita, wasap, ujumbe mfupi (SMS) na hata kupiga simu kwa wagombea na wengi naamini walijibiwa, yote hayo yaliongeza ukaribu baina ya wagombea na wapigakura.

"Si hivyo tu kukutana na makundi ni njia mojawapo ya kuendeleza uhuru wa kutoa maoni na kushauri pale inapoonekana kuna uhitaji...," anasema Munuo.

Kwa upande wake anaouna utaratibu wa kusikiliza wapigakura kuwa ni bora na unaohitaji kutumiwa zaidi siku zijazo ili kuongeza uwajibikaji wa watakaochaguliwa na ufuatiliaji wa ahadi kwa upande wa makundi ya walioahidiwa.

Ni njia bora kuliko na inafaa kuendelezwa na kudumishwa ili wagombea wawasikilize zaidi wapigakura badala ya kusikilizwa na wananchi muda wote.

KUFUNGIA KAMPENI

Kwa mara ya kwanza kwenye historia ya uchaguzi mkuu wapo waliofungiwa wakati wa kampeni kutokana na maelekezo yaliyotolewa na Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC) nao ni wagombea wa CHADEMA Tundu Lissu , anayegombea urais wa Jamhuri ya Muungano na Halima Mdee mgombea ubunge jimbo la Kawe, pamoja na mgombea urais Zanzibar Seif Sharif Hamad wa ACT Wazalendo.

Kilichowafanya wafunguwe kwa mujibu wa NEC ni kwa kufuatana na kanuni za maadili ya uchaguzi ambazo vyama na wadau ikiwamo serikali wamejiwekea kulinda amani wakati wa kampeni na kwamba lengo kushughulikia changamoto kama hizo.

Baadhi ya wadau wakizungumzia suala hilo wanasema nia ya kuwa na maadili hayo haikuwa mbaya licha ya kwamba wengine walikosoa hatua hiyo wakisema kuwa katika nchi nyingine hakuna utaratibu kama huo.

Baadhi ya wachambuzi wanasema siyo kila kitu kinachofanyika nchi nyinginezo kinafaa kwa Tanzania na pia siyo kila linalofanywa linafaa hapa nchini, hivyo kuigwa na mataifa mengine, bali wanaona kuwa kila nchi ina mipango yake na mbinu zake kufanikisha uchaguzi kuendana na sababu, mazingira ya kisiasa, utamaduni na changamoto zake ambazo hazifanani.

Sasa, swali ambalo linafaa kuulizwa ni je, kanuni hizo zinaweza kuchukuliwa kama chanzo cha kusababisha pengine washiriki kuona kuwa zinapunguza haki ya uhuru wa kutoa maoni, kukosoa na kuleta uelekeo mbadala wakati wa kampeni au kitu kinachostahili kudumishwa na kuboreshwa zaidi.

## JUKWAA LA UONGOZI

# KIBWAGIZO CHA MEMBE

## • Wiki moja ni muda mrefu kisiasa aliyagundua urais uliposambaratika



Wagombea urais Bernard Membe wa ACT-Wazalendo (kushoto mbele) na Tundu Lissu wa CHADEMA, wakipeana mikono kujipanga kufanikisha kampeni za uchaguzi mkuu unaofanyika leo . PICHA: MTANDAO.

**Na Ani Jozeni**

ALIKUWA ni Jenerali wa Ufaransa, Charles de Gaulle, kiongozi wa wanajeshi walioitoa nchi yao kwenye makucha ya kifashisti ya Wajerumani wakati wa vita vikuu vya pili vya dunia, aliyesema 'wiki moja muda mrefu katika siasa'.

Aliyasema hayo miaka iliyofuata akiwa kiongozi mkuu wa nchi hiyo. Kuthibitisha kuwa ni mhenga aliyeelewa mambo, watu waliokuwa hawataki aondoke madarakani kwa kutotaka kushiriki serikali za mseto (na vyama vya kimapinduzi), aliwatahadharisha kuwa hakuna ambaye atatamba kuwa bila yeye mambo yatakwama tu.

Katika kugombea uongozi nafasi yoyote, kuna hulka ambayo mtu binafsi anaijenga, kwa kutumia vigezo ambavyo inawezekana ni sahihi kwa kipindi kilichopo, lakini haviwezi kudumu kwa muda mrefu au vinaonekana kuendelea kudumu na halafu ghafla vinakwama. Ndivyo ilivyotokea kwa aliyekuwa mgombea wa ACT-Wazalendo Bernard Membe, aliyejitosa kwenye nafasi ya urais Muungano.

Membe, ambaye alikuwa na uhakika wa kuvuta watu wa kutosha kwake ,wajumbe wa NEC wakati wa uteuzi mwaka 2015, akiwa na uhakika kuwa wengine wangekatwa kwa tuhuma mbalimbali, asingejua kuwa unaweza kutokea mvutano wa huko kukatwa, akatafutwa mtu mwingine badala ya aliyependelewa na yule 'mkataji.'

Na kwa njia hiyo angetazamia pia kuwa baada ya kuwa kinara kufukuzwa katika chama tawala na huku akijua kuwa Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe aliwahi kuingia katika kinyang'anyiro cha urais akakwama, alidhani ndiye angefaa kuinua bendera upinzani.

Alifaulu hadi hapo, ila asingejua kuwa mbunge machachari Tundu Lissu, angethubutu kurudi mwisho wa Julai na akirudi 'ndio ule mwisho,' kuwa hakuna mshika bendera upinzani zaidi yake.

Ni kitu ambacho hakikufahamika kinagaubaga, hadi wakuu wa vyama upinzani wakaangalia watu wanavyokuja kampeni, wanachozungumza na nani wanamsikiliza pamoja na kumfuatilia.

Katika mazingira hayo, kukawa kuna ufa mkubwa kati ya alichotazamia Membe na kinachoonekana waziwazi na licha ya kuwa kanuni za uchaguzi mwaka huu zinamsaidia kubakisha jina lake katika karatasi ya kura, haikuwa sababu ya kutosha kwa chama chake kuendelea na kampeni isiyo na tija.

> “ Alifaulu hadi hapo, ila asingejua kuwa mbunge machachari Tundu Lissu, angethubutu kurudi mwisho wa Julai na akirudi 'ndio ule mwisho,' kuwa hakuna mshika bendera upinzani zaidi yake.

Suala hilo likaamuliwa 'kiaina' katika kikao cha pamoja ambacho mgombea huyo wa ACT-Wazalendo inasemekana alikuwepo.

Ikawa kama historia inajirudia, kuwa mwaka 2015 wagombea watarajiwa wa CUF na CHADEMA Lipumba na Dk. Wilbroad Slaa, walikuwepo katika kikao cha kumpitisha Edward Lowassa, lakini nafsi zikawasuta wakasepa.

Kwa njia hiyo Membe alijikuta nafsi inamsuta kuwa juhudi zote alizofanya na utaratibu mzima wa kampeni ulivyo, halafu ajitoe mwenyewe wakati jina lake litakuwa kwenye karatasi ya kura ni kitu ambacho kinaendelea kutafakariwa.

Mstaafu huyo wa Wizara ya Mambo ya Nje, akatafuta njia ya kuendelea na mpango wa kupiga kampeni wakati vyama vimeshakubaliana kuwa ni mgombea wa CHADEMA ndiye asimame apigiwe debe.

Pia kuna sura ya usiache mbachao kwa msala upitao, katika suala hilo, kwani mradi alishatumikia nafasi ya uwaziri miaka mingi na alikuwa chama tawala, anafahamu kwa undani nini kinaendelea serikalini, aliona vigezo vinatosha kwa kampeni.

Ndiyo hapo usemi wa pili wa de Gaulle unapokuja, kuwa hata kama mtu ni muhimu kiasi gani, chama chake kikishamkana hawezi tena kusimama mbele za watu akafanya jambo, kwani ni kama yeye ni mgombea binafsi asiyeruhusiwa kisheria au muasi aliyekataliwa na chama chake.

Chama ni kundi la marafiki linalotoa utambulisho kitaifa mgombea husika ni mtu wa aina gani, anadhaminiwa na nani na siyo ajilete vile anavyotaka.

Uendeshaji chama tayari ni shughuli ya kitaifa, ni muungano wa kizalendo ambao unampa mhusika sifa za kuzungumza kwa niaba ya wengi na mgombea akikampeni kivyake hajulikani anatokea wapi.

Ikilinganishwa na 2015, safari hii aliyetokea CCM ndiye aliyetakiwa kuacha azma ya kugombea kwani anayetoka upinzani ndiye mwenye nguvu ya angalau kupambana na CCM, wakati aliyetokea CCM.

Hakufika huko na jeshi lolote, hasa kwa vile aliondoka kutokana na matazamio yake na siyo hali ya madai yenye mashiko kiasi fulani ya kutotendewa haki, kama yule waliomtangulia walivyofanya.

Hivyo historia inajirudia ila siyo katika maazingira yanayofanana na mhenga mmoja akisema historia inapojirudia ,mara ya kwanza inakuwa mkasa, halafu baadaye ni mzaha.

Ndiyo tofauti ya ujuo wa Lowassa kupeperusha bendera ya CHADEMA uchaguzi mkuu uliopita na ujio wa Membe kuwakilisha upinzani akishikilia bendera ya ACT-Wazalendo uchaguzi mkuu wa sasa.

Halafu kuna suala jingine limejificha, kuwa kukwama ugombea urais wa Membe ni kielelezo kingine kuwa kuna tofauti kati ya chama na kukubalika kwa kiongozi mmoja au wawili katika chama hiki au kile.

Wakati Membe anaanza kuteta na Zitto Kabwe kupeperusha bendera ya chama chake, CHADEMA ilikuwa katika sononeko la kihistoria kutokana na mtafaruku ndani ya chama uliohusu uasi wa wabunge wa chama chake kwa sera au mkakati wa mwenyekiti Mbowe kuhusu corona.

Kurudi Lissu kukabatilisha masuala yote hayo, chama kikapata nguvu mpya.

Ni tukio jingine la historia kujirudia, kwa 'mkasa' wa ujio wa Lowassa halafu 'mzaha' wa kurudi Lissu, ambaye kabla ya madhila ya 'watu wasiojulikana' kumtwanga risasi zaidi ya 30 hakuwahi kuwa na sura ya 'mkombozi' wa chama na mpiga kampeni za urais.



## HABARI DODOMA

# Wanafunzi Kondoa wapata ukombozi kero ya usafiri

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

SHIRIKA la Compassion International Tanzania, limetoa msaada wa baiskeli 52 kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wilayani Kondoa Mkoa wa Dodoma, ambao wanatembea umbali wa zaidi ya kilometa sita kwenda shule.

Mkurugenzi wa kituo cha huduma ya mtoto AICT Pahi, Cosmas Rocket, alibainisha hayo jana kwenye hafla fupi ya kukabidhi msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni saba, iliyoambatana na kumuaga Askofu mstaafu wa Kanisa la AICT Dayosisi ya Pwani, Charles Salala.

Alibainisha baskeli hizo zitasaidia wanafunzi hao kufanya vizuri kitaaluma na kuondokana na vishawishi vitakavyokatisha ndoto zao.

Alisema, kutokana na wanafunzi wengi kutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilomita sita, kwenda na kurudi kila siku.

Mkurugenzi huyo alisema kutokana na hali hiyo kituo cha huduma kwa mtoto waliandaa andiko la kuomba msaada, ili kuwasaidia watoto hao.

"Msaada huu wa baiskeli kutoka Shirika la Compassion International Tanzania, utawasaidia watoto ambao wamekuwa wakilazimika kutembea umbali wa zaidi kilomita tatu kwenda shule, ili kuwapunguzia uchovu wa safari," alisema Rocket.

**Pia tunakabiliwa na tatizo la madarasa ya kutosha kwa ajili ya watoto wa madarasa ya chekechea na huduma ya mtoto, siku ya Jumamosi japo kanisa limejitahidi kujenga vyumba vya madarasa mawili ambayo bado hayajakamilika.**

Alisema pamoja na msaada huo wa baiskeli, lakini watoto kutoka kaya zenye mahitaji ya malazi wamepatiwa magodoro 15, ambapo kila moja limegharimu kiasi cha Sh. 150,000.

Mary Masala, kutoka kitengo cha huduma ya mama na mtoto akisoma risala ya kituo hicho cha AICT Pahi, alisema pamoja na mafanikio mbalimbali bado wanakabiliwa na tatizo la uchakavu wa mabweni katika Shule ya Wasichana Tana.

"Pia tunakabiliwa na tatizo la madarasa ya kutosha kwa ajili ya watoto wa madarasa ya chekechea na huduma ya mtoto, siku ya Jumamosi japo kanisa limejitahidi kujenga vyumba vya madarasa mawili ambayo bado hayajakamilika," alieleza Masala.

Naye Modesta Luvanda, Mwezeshaji Kanda ya Kati (PF) kutoka shirika hilo, aliwataka wazazi wa wanafunzi wilayani Kondoa kuacha tabia ya kuwalazimisha kufanya vibaya katika masomo yao.

"Wazazi lazima tuwasimamie watoto wetu ili wafanye vizuri katika masomo yao na kutimiza ndoto zao na si kuwa kikwazo cha kuwakwamisha katika safari yao kupata elimu, katika watoto hawa ambao wanalelewa na Compassion nisingependa kuona mtoto anaishia darasa la saba," alisema Luvanda.

Kwa upande wake, Askofu mstaafu wa Kanisa hilo, Charles Salala, alisema kuwa ipo haja ya jamii kubadili mitazamo yao ili kufikia maendeleo ya kweli.

Askofu Salala, alisema kuwa maendeleo ya kweli yanaletwa na Watanzania wenyewe na siyo kutegemea msaada kutoka mataifa mengine.

"Rai ni Watanzania tunatakiwa kubadilika katika fikra zetu na kuacha kuishi katika mazoea kwani pamoja na serikali kuboresha vitu mbalimbali ikiwamo miundombinu, ununuzi wa ndege, lakini maendeleo hayawezi kuja kama mitazamo ya jamii itabaki kama ilivyo sasa," alisema.

Aliwataka wazazi nchini kusimamia malezi ya watoto toka wakiwa wadogo ili kuwajengea misingi bora ya elimu na malezi.



Askofu mstaafu wa Kanisa la AICT Dayosisi ya Pwani, Charles Salala (kushoto), akizungumza na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wilayani Kondoa, pamoja na wazazi wao, baada ya kuwakabidhi msaada wa baiskeli kutoka Shirika la Compassion International Tanzania, mkoani Dodoma jana, ili kuwawezesha kuwahi shuleni kutokana na kuishi mbali. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Baraza la vyama lasisitiza amani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IKIWA leo Watanzania watafanya maamuzi ya kuchagua viongozi wa ngazi ya urais, ubunge na udiwani, Baraza la Vyama vya Siasa, limetaka kuzingatia amani na utulivu uliopo ili Tanzania iendelee kuwa kisiwa cha amani.

Vilevile, wagombea wameaswa kujiandaa kisaikolojia na kukubali matokeo yatakayotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ili kuepusha vurugu zitakazosababisha uvunjifu wa amani.

Mwenyekiti wa baraza hilo, John Shibuda, alitoa rai hiyo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alieleza wagombea wote wanapaswa kujiandaa kisaikolojia na wawe tayari kupokea matokeo ya ushindi au kushindwa.

Alisema kila mgombea anapaswa kukubali somo kuwa asiyekubali kushindwa siyo mshindani na asiyekubali subra za kuongozwa na mwenzake hana sifa za kuitwa kiongozi wa jamii.

"Washindani wote wa nafasi za kushika mamlaka ya dola mkumbuke kuwa siasa sio imani za kidini za kuenzi nguzo kuu kwa Utukufu wa Mwenyezi Mungu, hivyo wanasiasa tuache kufarakana kwa mambo yasiyo na thawabu kwake, wote tukumbuke usemi usemao kuvunjika kwa jembe siyo mwisho wa uhunzi," alisema Shibuda ambaye anagombea urais kupitia Chama cha ADA-TADEA.

Shibuda ambaye hakufanya kampeni za majukwaani, alieleza kuwa ni vyema busara za wanasiasa na busara za mashabiki wa vyama vyote zikatambua kuwa kura za ushindi hazitatokana na kigezo cha taswira ya hadhara zilivyokuwa katika vipindi vya mwitikio wa mahudhurio ya wasikilizaji wa mikutano ya kampeni.

"Kama ambavyo Simba na Yanga hupeana mikono baada ya kutifuana katika kushindania ubingwa wa Taifa ndio hivyo hivyo na sisi tupongezane kwa kutakiana heri kwa matokeo kutokana na maamuzi matamu ama kupatikana matokeo machungu ya utashi wa umma yatakayotolewa na Tume."

Aliongeza: "Maajabu ya siku ya kupigwa kura hutoa somo ambalo lina jawabu la jibu lisemalo kuwapo umati wa watu wengi katika mikutano ya kampeni siyo nyenzo ya matokeo ya tarakimu halisia za namba za takwimu za hesabu za idadi ya wapigakura za ndio na za kutoa ushindi."

**Kila mgombea anapaswa kukubali somo kuwa asiyekubali kushindwa siyo mshindani na asiyekubali subra za kuongozwa na mwenzake hana sifa za kuitwa kiongozi wa jamii.**

# Watakiwa kuzingatia sheria za masoko

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Masoko wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, James Yuna, ametaka makundi ya wafanyabiashara wadogo (machinga) kuzingatia sheria ndogo za masoko kwenye majukumu yao.

Yuna aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na makundi hayo kwenye masoko yaliyopo ndani ya jijini hapa.

Alisema masoko bado yana nafasi za kufanya biashara mbalimbali zikiwamo za mamalishe, hivyo hakuna sababu za kuvutana na halmashauri kwa kufanya biashara zao kwenye maeneo yasiyo rasmi.

"Hatuna sababu ya kuvutana kati yetu na makundi yaliyopo ya wafanyabiashara kuhusu ufanyaji wenu wa biashara, kinachotakiwa kila mmoja asimame kwenye nafasi yake, ili kuleta ufanisi pande zote mbili lengo likiwa kuinuana kiuchumi kwa upande wenu," alisema.

Alibainisha kuwa bado kuna baadhi ya makundi ya wamachinga yanakiuka taratibu za Jiji.

Naye mamalishe wa Soko la Sabasaba, Mwanahamisi Yusuph, alisema wamekuwa wakizingatia maagizo ya Jiji, hatua ambayo imesaidia kufanya biashara zao bila kubugudhiwa.

Alisema wamekuwa wakitunza mazingira na ufanyaji biashara kwenye maeneo rasmi, imechangia kujikwamua kiuchumi na usalama wa afya za walaji.

"Tunaishukuru Halmashauri ya Jiji kwa kutuwezesha elimu ya kufanya biashara zetu bila kubughudhiwa, hii ni baada ya kufuata kanuni, sheria na kuweka mazingira katika hali ya usafi," alisema.

Kwa upande wake, mfanyabiashara Hashimu Hussen wa Soko la Miembeni, alisema uwapo wa kitambulisho cha mjasiriamali kimesaidia kuwapa uhuru na kufanya kazi bila kuvunja sheria zilizopo.

"Pia wamachinga wengi hivi sasa biashara zao zimekuwa zikifanywa kwa ushindani wa soko kwa kuboresha, hii ni baada ya kupatiwa maelekezo kutoka Jiji," alisema.



# Wakulima wapewa uhuru kuamua bei

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KAIMU Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Francis Alfred, amesema wakulima wa zao hilo ndio wenye uamuzi wa mwisho kuuza korosho baada ya kuridhika na bei inayopendekezwa na wanunuzi kwenye minada mbalimbali inayoendelea.

Alfred alisema hayo jana wakati wa mkutano na wanahabari jijini hapa kwamba kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani, serikali haitawapangia wakulima wala wanunuzi bei badala yake itaendelea kutoa mwongozo kulingana na soko la dunia.

Mkurugenzi huyo alisema lengo kuu la miongozo hiyo ni kuweka ushindani katika masoko ya minada mbalimbali ya korosho na kwamba uamuzi wa kuuza au kutokuuza uko mikononi mwa wakulima wenyewe.

**Sisi bodi tunahakikisha tunaongeza ushindani wa soko kwa kuhakikisha tunaweka ushindani wa masoko ya minada ili wanunuzi wanunue kwa bei elekezi...**

"Sisi bodi tunahakikisha tunaongeza ushindani wa soko kwa kuhakikisha tunaweka ushindani wa masoko ya minada ili wanunuzi wanunue kwa bei elekezi ya kumnufaisha mkulima kuliko ununuzi holela," alisema.

Kuhusu Kituo cha Mnada cha Tunduru kukataa kuuza korosho kuwa si cha kulalamikiwa bali ni uamuzi uliofikiwa na wakulima kwa madai hakuna sheria inayowabana, hivyo waliamua kuuza kwa wakati mwingine watakaoona bei ya zao ni nzuri.

Alfred alisema uzoefu unaonyesha kuwa zinapokaribia sikukuu cha Krismasi na Mwaka Mpya, bei za korosho hushuka na kushauri wakati mzuri wa kuuza ni mapema Januari, muda ambao bei huwa nzuri.

Msimu wa sikukuu za kumaliza mwaka, alisema wakulima wengi huondoka mashambani, hivyo huamua kuuza korosho kwa bei ya hasara. Kutokana na hali hiyo, alishauri wakulima kuwa wavumilivu na kusubiri mwanzo wa mwaka mwingine kuuza kwa bei nzuri.

Mratibu wa CBT kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo (TARI) Naliendele, Dk. Geradina Mzena, alisema wakulima wanapaswa kuzingatia ubora wa uzalishaji wa zao hilo.

Alisema kwa kuzingatia kanuni za kisasa katika upandaji, utunzaji na uvunaji wa zao hilo ili kusaidia kupata mavuno mazuri ambayo yatamudu soko la ushindani ndani na nje ya nchi.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), akibadilishana mawazo na waendesha bodaboda katika moja ya vijiwe vya Kata ya Iyela, jijini humo juzi, alipokuwa kwenye ziara ya kukagua miundombinu ya barabara. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Dk. Tulia atamba kuiboresha Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Mbeya Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Tulia Ackson, ameahidi kuboresha miundombinu ya maji na barabara, afya na elimu kwa kata zote 36 za Halmashauri ya Jiji la Mbeya endapo leo atachaguliwa.

Pia amewaomba wananchi wa jimbo hilo kupitia sanduku la kura kumchagua ili ahadi hizo azitimize na kuwaletea maendeleo wananchi.

Dk. Tulia aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe akieleza vipaumbele alivyoviweka kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/25 endapo atachaguliwa kuwa mwakilishi wa wananchi kupitia jimbo hilo.

"Mimi ni mbunge ambaye natulia bungeni, naombeni ridhaa ya kwenda kuwawakilisha nikazishughulikie hizi kero za barabara za mitaa, maji, elimu na hata afya kwa sababu tayari ninayo 'koneksheni'," alisema Tulia.

Alisema matamanio yake ni kuomba Mbeya inapendeza na kuvutia kwa kujengwa barabara safi za mitaa wananchi kupata huduma safi za maji, matibabu ya uhakika na watoto kusoma kwenye mazingira mazuri na yenye utulivu, lakini uwepo wa shule katika kila kata za mitaa kwa shule za msingi na sekondari.

Alisema wananchi hawahitaji nguvu kubwa kufahamu masuala mbalimbali ya maendeleo aliyayafanya kwa wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini katika kuwaletea maendeleo ikiwamo mikopo ya bodaboda na bajaji, vikundi kukopeshwa ujenzi wa shule na vituo vya afya.

Alisema shughuli hizo zimechangia hali ya usalama na utulivu kwa vijana kwani tabia za wizi zimepungua kundi hilo sasa liko bize na shughuli za kujitafutia ridhiki kupitia mikopo waliyokopeshwa na Taasisi ya Tulia Trust.

Mgombea ubunge Jimbo la Mbarali kupitia CCM, Francis Mtega, aliwaahidi Wanambarali kuwa endapo atachaguliwa leo atatimiza ahadi zote alizoziahidi ikiwamo gharama nafuu ya ruzuku za pembejeo kwa wakulima.

Alisema tatizo ya pembejeo za kilimo kwa wakulima wa Mbarali ni sugu hali inayosababisha kuchelewa kuanza msimu mpya wa kilimo na kupata mavuno kidogo.

Alisema kero hilo ataifikisha katika vikao vya bunge, ili kuangalia namna bora ya kuwahisha mbolea na mahitaji mengi ya kilimo cha mpunga na kuwawezesha kulima kwa tija na waweze kunufaika vilevile aliwaahidi kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji kwa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya malisho.

# Viongozi wa dini wataka amani uchaguzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KAMATI ya Amani ya Mkoa wa Mbeya inayoundwa na viongozi wa dini zote imetoa tamko la kuomba Watanzania kudumisha amani wakati huu wa uchaguzi mkuu na kuiendeleza baada ya kumalizika kwa uchaguzi.

Hayo yalibainishwa jana na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Sheikh Mohamed Mwansasu, wakati wa kongamano la kuliombea taifa uchaguzi wa leo ufanyike kwa amani, lakini hata baada ya uchuguzi amani iendelee kuwapo.

Sheikh Mwansasu alitoa tamko kuwa wanahitaji amani iendelee baada ya uchaguzi kwa kuwa ndiyo tunu pekee inayounganisha maendeleo ya wananchi.

"Wakati huu ambao tunaanza kushiriki kupiga kura kuwa nawaomba Watanzania na wana Mbeya kwa ujumla kufanya uchaguzi kwa amani. Tuepuke vurugu na mapigano huku tukisubiri matokeo kutangazwa na baada ya hapo kuna maisha baada ya uchaguzi," alisema Mwansasu.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Padri Gasper Mwangoka, alikemea tabia ya vijana kuwaibia wazee kadi zao za kupigia kura ili washiriki kupiga kura kwa madai kuwa kwa kufanya hivyo ni kuwanyima haki ya kuchagua au kuchaguliwa.

Alisema baadhi ya wazee walisema vijana wao wanawarubuni kuwa wanahitaji vitambulisho vyao ili wakawapigie kura jambo ambalo ni kinyume na taratibu za tume ya uchaguzi.

Naye Katibu wa Kamati, Askofu Dk. Edward Mwaikali, akidai kuwa ana imani wananchi watailinda amani kwenye uchaguzi huu na baada ya kukamilisha kwa kuwa kila mara walitoa hamasa madhabahuni.

Alisema licha ya kuhubiri amani madhabahuni, pia waimbaji wa muziki wa injili walikuwa na jukumu la kutunga maudhui ya namna hiyo lengo likiwa kufikisha ujumbe.

Baadhi ya wajumbe walisema moja ya sababu zinazoifanya nchi kuendelea kuwa na amani ni kuheshimu sheria za nchi kwa kuhakikisha kila mtu anatimiza wajibu wake bila kuingilia mipaka ya vyombo vya sheria.



HABARI ZANZIBAR

# Wengi wajitokeza kura ya mapema

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

UPIGAJI kura wa mapema ulifanyika jana katika maeneo yote ya vituo 407 yaliyopangwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), idadi kubwa ya wapigakura wanaohusika na walioomba kushiriki, walijitokeza kwa wingi vituoni.

Mkurugenzi wa ZEC, Thabit Idarous Faina, wakati akitembelea katika vituo vya kupigia kura alisema wapigakura walijitokeza kwa wingi kutokana na Tume kujiandaa vizuri katika kufanikisha kura hiyo.

Alisema zoezi hilo lipo kisheria na linawahusu wapigakura maalum walioainishwa katika Sheria ya Uchaguzi Na. 4 ya mwaka 2018 kifungu cha 82(2)(a)(b) na kuwaasa wale ambao hawakutajwa katika kifungu hicho kubaki nyumbani na badala yake wasubiri hadi leo.

Mkurugenzi huyo alisema kwa mujibu wa utaratibu wa kura ya mapema mawakala wa vyama vya siasa baada ya kukamilika upigaji kura wataweka lakiri (vifungio) vyenye namba maalum katika masanduku ya kura, ili kuhifadhi na kulinda usalama wa kura zilizopigwa.

Hata hivyo, Mkurugenzi Faina aliviasa vyombo vya habari vinavyoripoti matukio ya uchaguzi kutoripoti matokeo ya idadi ya kura zilizopigwa kwani mwenye jukumu la kufanya hivyo ni ZEC.

Akizungumzia hali ya utulivu katika vituo vya kupigia kura, Kamanda wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Awadhi Juma Haji, aliwatoa hofu wananchi kuwa hali ya ulinzi na usalama imeimarika katika vituo vyote vya kupigia kura, ambapo Jeshi la Polisi limejipanga kuendelea kuimarisha katika maeneo yote Zanzibar na kuwadhibiti wale wote wanaotaka kujaribu kuivuruga amani nchini.

Baadhi ya wapigakura ya mapema waliofika vituoni kupigakura, walisema, utaratibu uliotumika kuendesha kura ya mapema ni mzuri na waliwasisitiza wananchi kuzifuata sheria na taratibu zilizowekwa na Tume, ili kufanikisha zoezi la uchaguzi katika hali ya amani na utulivu.

Tume inatarajia kuendesha upigaji kura wa pamoja leo kwa wapigakura waliomo katika daftari la kudumu la wapigakura ambao hawakupiga kura ya mapema.

# Balozi Iddi awaachia ujumbe watumishi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema mtumishi wa taasisi ya umma na binafsi katika ngazi yoyote anapaswa kuzingatia dhima ya kutekeleza wajibu wake katika kuutumikia umma ili pale atakapoondoka aache athari itakayoendelea kuleta tija na kukumbukwa muda wote.

Alisema zipo sifa za baadhi ya watumishi katika sehemu za kazi ambazo hubakia kuwa kielelezo cha utumishi uliotukuka na wakati mwingine husaidia hata jamii pale inapohitaji huduma katika sehemu hizo au fursa za ajira, jambo ambalo humjengea historia ya kudumu katika mioyo ya jamii.

Balozi Iddi alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na watendaji wa taasisi zilizo chini ya Ofisi yake kwa upande wa Pemba, kikao ambacho kimefanyika Pagali Chake Chake Pemba na kwa Unguja kilifanyika Kikwajuni akiwaaga baada ya kufanyakazi nao pamoja katika kipindi cha utumishi wake wa miaka 10 akiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Alisema jamii imekuwa ikishuhudia vituko vya baadhi ya watumishi wa umma katika ngazi tofauti wanaolalamikiwa kutokana na tabia yao mbaya katika kuwahudumia wananchi na matokeo yake watu hushangilia na wengine kudiriki hata kupita chakula kitamu kujipongeza kutokana na kuondoka kwake katika jukumu husika.

**Kusameheana ndani ya uwajibikaji baina ya watendaji katika sehemu za kazi ni sifa na falsafa inayofuta chuki, kero na maonevu mambo yanayonyoosha ustawi wa jamii.**

Balozi Iddi aliwakumbusha watendaji hao licha ya mabadiliko ya uongozi wa juu yanayofanyika kutokana na sheria, kujiepusha na tabia ya majungu, dhana mbaya, fitina na hata kusengenyana, mambo ambayo alisema yanayochangia kuzorotesha uwajibikaji wao unaotarajiwa na wananchi.

Aliwashukuru na kuwapongeza wafanyakazi wote wa idara ya falagha kutokana na mchango mkubwa waliompa uliomuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Balozi Iddi alisema wakati tameshaamua kustaafu, baada ya kutoa mchango wake mkubwa ndani ya Serikali zote mbili na Chama Cha Mapinduzi tokea mwaka 1965, aliwaomba watendaji hao kuendelea kutoa ushirikiano kwa kiongozi mwingine mpya atakayewasimamia ili kutimiza matarajio ya wananchi.

"Nimeamua kustaafu baada ya kutoa mchango mkubwa wa Serikali na CCM kwa muda mrefu tokea Mwaka 1965 nilipoanza na kazi ya ualimu, baadae afisa wa wizara ya mambo ya nje, nafasi ya diplomasia na hatimae siasa. Kiongozi mzuri Mtu asisubiri kufukuzwa," alisema Balozi Iddi.

Katika risala yao watendaji na wasaidizi hao wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Pemba na Unguja walisema mambo mengi ya mafanikio yaliyopatikana ndani ya miaka 10 ni msingi mzuri wa Balozi Iddi.

Walisema kipindi chake kimemuwezesha kusimamia mambo mengi yaliyoleta tija na hatimae taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar zikatekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mohamed Aboud Mohamed, aliwaomba watendaji na wasaidizi hao kuendelea kupendana na hiyo ndio sifa ya ufanisi mzuri wa majukumu ya watumishi katika kutumikia umma.

Waziri Aboud alisema yapo upungufu mdogo unaomkumba mtumishi wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, lakini kinachozingatiwa na kutiwa maanani ni suala la uvumilivu likiwa chachu ya kupata maendeleo ya haraka.

Alibainisha kwamba kusameheana ndani ya uwajibikaji baina ya watendaji katika sehemu za kazi ni sifa na falsafa inayofuta chuki, kero na maonevu mambo yanayonyoosha ustawi wa jamii.



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mwanamwema Shein, akitia ubani katika chetezo kuashiria kufungua kisomo cha dua ya kuitakia amani nchi kipindi cha uchaguzi mkuu na baada ya uchaguzi, iliyoandaliwa na Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), jijini Zanzibar juzi. Kushoto kwake ni Makamu Mwenyekiti wa UWT, Thuwaiba Editon Kisasi na (wa tatu kulia) ni Mke wa Mgombea Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, mama Maryam Mwinyi. **PICHA: IKULU**

# Mahujaji walioahirisha safari ya hija wapewa ushauri

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAUMINI wa dini ya Kiislamu ambao hawakwenda kwenye ibada ya Hija katika Mji mtukufu wa Maka nchini Saudi Arabia mwaka huu, wametakiwa kuwa na nia hiyo hadi ugonjwa wa corona utakapoisha.

Ushauri huo ulitolewa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, na kueleza kuwa hadi sasa zipo baadhi ya nchi zinaendelea kuzuia raia wao kusafiri nje ya mataifa yao na kutoruhusu wageni kuingia kwenye nchi hizo kutokana na janga hilo lililogharimu maisha ya watu wengi na kuacha taharuki.

Balozi Iddi alisema hayo wakati akizungumza na mahujaji watarajiwa kwenye ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdulwakili Kikwajuni, kikao alicho alikitumia kuwaaga rasmi akikamilisha muda wake wa utumishi wa Serikali .

Aliwataka mahujaji watarajiwa hao kutoona machungu kutokana na matukio hayo ya kuzuka kwa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona na dunia haijakaa salama kutokana na janga hilo.

Aidha aliwakumbusha wananchi kuzingatia umuhimu wa kutekeleza masharti yote yaliyowekwa na wataalamu wa afya katika mapambano dhidi ya virusi vya corona ili visirejee tena katika ardhi ya Tanzania. Alisema wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla wanachokihitaji kabla na baada ya uchaguzi mkuu ni kuona maisha yao yanaendelea kama kawaida bila ya wasiwasi katika muelekeo wa misingi ya amani na utulivu waliouzoea.

Akitoa maelezo ya mwenendo wa mahujaji hao watarajiwa, Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar, Khamis Juma Maalim, alisema Zanzibar ina taasisi 23 zinazosafirisha mahujaji kwenda kutekeleza ibada ya Hijja Maka nchini Saudi Arabia.

Khamis alisema mahujaji watarajiwa 1,600 walijiandikisha mwaka jana katika taasisi 19 ambapo jumla ya mahujaji 933 wamewahi kukamilisha gharama za malipo kwa ajili ya safari hiyo ya kidini.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar, Sheikh Abdullah Talib Abdullah, alimpongeza Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa jitihada zake zilizosaidia uratibu mzuru katika usimamizi wa Ibada ya Hija.

Sheikh Talib alisema jitihada hizo ndizo zilizosaidia kuibuliwa kwa wazo la kuanzishwa kwa mfuko wa Hija Zanzibar ambao tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaidhia jambo hilo muhimu kwa mustakabali wa ibada ya Hija ambayo ni nguzo ya mwisho ya uislamu inayomuwajibikia muumini mwenye uwezo kuitekeleza.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

**SHAMBA L INAUZWA LIPO KIBAHA KONGOWE** Shamba linauzwa lenye ekari 10 Tsh 25,000,000 lipo kibaha kongowe umbali kutoka barabarani hadi shamba KM 9 Kwa mawasiliano zaidi 0754826580.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo **MJINI-MOROGORO**
Usimamizi wa mirathi No;310/2020
Ombi la **SALIMA MICHAEL MGANGA** ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **PERPETUA HASSAN.**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **02/11/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **15/10/2020.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo MIKESE.
Usimamizi wa mirathi No;05/2020
Ombi la **PETER NEJI MAGUNGULI** ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **EMERITHA FIVAWO MAGUNGULI.**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **03/11/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **08/10/2020.**

**TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

MAHAMUD JAHA SERWENDWA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 510 CJH AINA YA NISSAN PATROL YENYE CHASIS NO **LBRSPJB55J9018859NA** ENGINE NO **SLI57FMII8922214** KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KA **H/RB//6112/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya Mwanzo ya **CHAMWINO MJINI**
Usimamizi wa Mirathi 97/2020.
Ombi la **HASSANI MOHAMED** kuteuliwa kuwa
Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **MOHAMED THABIT MOHAMMAD**
KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe **09/11/2020** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Tarehe **22/10/2020.**


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**






TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA




Donald Trump akiwa na Jaji Mkuu mpya. **PICHA: MTANDAO**

# Kenyatta azindua ripoti rasmi ya maridhiano

**NAIROBI,** Kenya

RAIS Uhuru Kenyatta na Waziri Mkuu wa zamani nchini Kenya Raila Odinga, wamezindua rasmi ripoti ya maridhiano, maarufu kama BBI inayolenga kuwapatanisha wakenya wote bila kujali makabila yao.

Rais Uhuru Kenyatta aliwalaumu viongozi kwa kuchangia kuongezeka kwa ukabila nchini humo na kwamba iwapo suala la ukabila halitachukuliwa kwa uangalifu, huenda likawa bomu litakalolipuka.

Safari ya kufanyika kwa kura ya maoni nchini Kenya, ilianza rasmi jana wakati zaidi ya wakenya 6,000 walipojumuika katika ukumbi wa Bomas jijini Nairobi, kwenye uzinduzi wa ripoti ya maridhiano ya BBI.

Ripoti hiyo ambayo imekuwa ikitayarishwa kwa kipindi cha miaka miwili sasa, na ambayo imewafurahisha viongozi wote waliopata nafasi ya kuhutubia, inapendekeza marekebisho kwenye muundo wa utawala wa serikali.

**Kinyume na katiba iliyopitishwa mwaka 2010, ripoti ya BBI inapendekeza ofisi ya kiongozi wa upinzani ambaye atawajibisha serikali.**

Ripoti hiyo inapendekeza kuwepo kwa nafasi za Waziri Mkuu na manaibu wake wawili na waasisi wake wanasema sababu kubwa ni kuzima ghasia za kila baada ya Uchaguzi Mkuu.

Rais Uhuru Kenyatta (pichani) alimtaka Naibu wake Ruto kupunguza kampeni za siasa kabla ya uchaguzi mkuu ujao.

Hata hivyo, baadhi ya wachanganuzi wa siasa walisema mapendekezo ya ripoti ya BBI yanampa rais mamlaka zaidi, kwani atakuwa na uwezo wa kumchagua na kumfuta kazi Waziri Mkuu.

Aidha, wapinzani wa ripoti hiyo walisema kuongezwa kwa nafasi za uongozi kutaongeza mzigo kwa walipa kodi.

Aidha, ripoti hiyo imependekeza kuboreshwa kwa serikali za majimbo kwa kuongeza mgawo kwa asilimia 35 kutoka kwa asilimia 15 huku uwakilishi wa wanawake ukipigiwa debe kwenye ripoti hiyo.



Katika majimbo 47, watachaguliwa maseneta wawili mmoja wa kike na mwingine wa kiume, huku gavana wa kiume akihitajika kumchagua naibu wa kike.

Raila Odinga aliwataka wakenya kukabiliana na ugonjwa wa ukabila, ambao alisema umekuwa ukilitafuna taifa hasa wakati wa uchaguzi.

Mapendekezo mengine kwenye ripoti hiyo ni kuwapo kwa Waziri Mkuu, ambaye atakuwa kiongozi wa bunge na baraza la mawaziri kwa niaba ya serikali.

Kinyume na katiba iliyopitishwa mwaka 2010, ripoti ya BBI inapendekeza ofisi ya kiongozi wa upinzani ambaye atawajibisha serikali.

Kiongozi wa upinzani atakuwa mgombea wa pili kwenye uchaguzi mkuu ama atachaguliwa kutoka kwa muungano wa vyama wenye asilimia 25 ya wabunge wote.

Mchakato wa Ripoti hiyo ulianza wakati Rais Kenyatta na Raila walipoamua kuzika tofauti zao za siasa kwenye uchaguzi uliokumbwa na mvutano mwaka 2017, katika kile kilichoitwa kupeana mkono.

## Umoja wa Mataifa wasema Yemen ina hali ngumu

**SANAA,** Yemen

RIPOTI ya Umoja wa Mataifa iliyotolewa jana imeeleza kwamba sehemu za Yemen zinakabiliwa na kiwango kikubwa cha utapiamlo kwa watoto na kuongeza tahadhari kwamba nchi hiyo inaelekea kwenye baa kubwa la mgogoro wa usalama wa chakula.

Vichocheo vya utapiamlo nchini Yemen vimeongezeka katika mwaka 2020 wakati janga la virusi vya Corona, kushuka kwa uchumi, mafuriko, kuongezeka kwa mgogoro na ufadhili mdogo wa shughuli za msaada mwaka huu vikizidisha hali ya njaa nchini humo baada ya takriban miaka sita ya vita.



Mratibu wa shirika linalohusika na masuala ya kibinadamu kwa ajili ya Yemen, Lise Grande alisema tangu mwezi Julai wameonya kwamba Yemen inakaribia kutumbukia kwenye janga kubwa la mgogoro wa usalama wa chakula.

Aliongeza kuwa ikiwa vita havitamalizwa hivi sasa katika taifa hilo basi itaelekea kwenye hali ambayo haitaweza kubadilishwa na kuingia kwenye hatari ya kupoteza kizazi kizima cha watoto nchini humo.

# Jaji Mkuu athibitishwa na Seneti

**WASHINGTON,** Marekani

AMY Coney Barret, amethibitishwa na Baraza la lililogawanyika la Seneti kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Marekani.

Hilo limewezekana baada ya wanachama wa Republican kuwashinda nguvu Democrat na kumwidhinisha mteule huyo wa Rais Donald Trump kabla ya uchaguzi.

Hatua hiyo huenda ikawapa wahafidhina wingi wa majaji katika mahakama hiyo kwa miaka kadhaa ijayo.

Barret ambaye ni chaguo la Trump kujaza nafasi ya mliberali Ruth Bader Ginsburg aliyefariki, anafungua enzi mpya za hukumu kuhusu utoaji mimba, sheria ya bima ya afya na hata uchaguzi wake mwenyewe.

Wademocrat walishindwa kuzuia matokeo, ambayo ni jaji wa tatu wa Trump kwenye mahakama hiyo wakati warepublican wakishinda mbio za kuiunda upya mahakama hiyo.

# MADRID YAKOMAA NA POCHETTINO



**MADRID,** Hispania

LICHA ya kupata ushindi katika mchezo wa Classico dhidi ya Barcelona, ripoti za ndani kutoka kikosi cha Real Madrid zinadai uongozi wa miamba hiyo upo kwenye harakati za kutaka kumchukua kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino.

Pochettino anatajwa kwamba anaonekana kufiti zaidi kuchukua mikoba ya Zinedine Zidane ambaye yupo hatarini kufukuzwa kutokana na mwenendo wa matokeo mabaya wanayoyapata.

Real Madrid ilipoteza michezo miwili ya mwisho kabla ya mechi ya Barcelona ikiwa ni baada ya ule wa Ligi ya Mabingwa dhidi ya Shakhtar Donetsk ilipofungwa mabao 3-2, sambamba na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Cadiz, ambapo ilikubali kichapo cha bao 1-0.

Ripoti zilizochapishwa kwenye tovuti ya SunSport zinadai Real Madrid imewaweka kwenye rada Pochettino na mkongwe wa klabu hiyo, Raul kama mbadala wa Zidane.

Lakini Pochettino ndiye anaonekana kuwa kwenye nafasi kubwa zaidi ya kusainishwa kutokana na uzoefu wake na mafanikio aliyoyapata tofauti na ilivyo kwa Raul.

Pochettino hana timu ya kufundisha tangu Novemba mwaka jana baada ya kufutwa kazi na Spurs kutokana na matokeo mabovu ya timu hiyo, ikiwa ni miezi michache baada ya kuifikisha kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa ambapo ilipoteza dhidi ya Liverpool.

# Martinez azungumzia majaliwa yake




**MILAN,** Italia

LAUTARO Martinez amesema ana furaha pale Inter Milan, lakini "hajui nini kitatokea kesho" kauli hiyo akiitoa wakati akizungumzia majaliwa yake hapo katika klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Martinez amekuwa akihusishwa sana na mpango wa kuhamia kwa miamba wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Barcelona, ingawa straika huyo wa Inter amebakia pale Milan.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye amefunga mabao matano kwenye Ligi Kuu msimu huu, aliulizwa kuhusu majaliwa yake hapo Milan kabla ya mchezo wa jana, Jumanne wa Ligi ya Mabingwa Uaya dhidi ya Shakhtar Donetsk.

"Nilijituma sana kila siku ili kujiimarisha zaidi," alisema Martinez akiwaambia waandishi wa habari.

"Nataka kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kuitumia vizuri klabu yangu pamoja na wachezaji wenzangu wa Inter Milan.

"Nina furaha hapa Inter. Tunafanya kazi kubwa kwa sababu tunataka kushinda mataji zaidi na Inter.

"Hiki ndicho ninachokifikiria leo hii. Sijui nini kitatoke kesho, lakini naweza kuwaambia kwamba nina furaha hapa Inter."

# Klopp hajui lini Van Dijk atarejea

**LIVERPOOL** England

KOCHA wa Liverpool amesisitiza kwamba beki wa kati Virgil van Dijk, anaendelea na matibabu na hakuna taarifa kamili juu ya lini anaweza kuwa sawa akiongeza kwamba majeraha yake hadi kupona yatachukua muda mrefu.

Beki huyo wa Liverpool alipata majeraha katika mchezo dhidi ya Everton baada ya kukumbana na kipa wa timu hiyo, Jordan Pickford wiki iliyopita na ripoti ambazo hazikuthibitishwa zilidai atakaa nje kwa miezi nane au saba.

Suala hilo linazidi kumuumiza kichwa kocha huyo kwa kuwa Van Dijk kwake ni miongoni mwa wachezaji muhimu wa kikosi cha kwanza ambaye uwapo wake ulikuwa unaifanya safu ya ulinzi ya Liverpool kuwa imara zaidi.

Licha ya nafasi yake kuchukuliwa na Fabinho ambaye alionyesha kiwango kikubwa katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa dhidi ya Ajax wakati ikishinda kwa bao 1-0, mambo yalionekana kuwa sio katika mchezo uliopita.

"Nafahamu kwamba mashabiki wengi wanapenda kumwona Virgil akiwa anacheza. Upasuaji utafanyika katika muda maalumu uliopangwa na wala hatuwezi kusema atacheza baada ya muda gani kwa kuwa watu wanatofautiana kwenye kupona," alisema.

Fabinho ambaye anatumiwa kama mbadala wa beki huyo Mholanzi na kuonekana anaweza kuifanyia kazi vizuri eneo hilo, mchezo uliopita dhidi ya Sheffield United alionyesha kuwa na makosa mengi ikiwa pamoja na lile la kumchezea vibaya Oli McBurnie na kusababisha mwamuzi kuipa penalti Sheffield.

Lakini Klopp alimtetea na kusisitiza, refa wa mchezo huo hakuwa sahihi akiongeza kwake haikuwa penalti wala faulo.

"Ilikuwa ni katika harakati za kuuwania mpira. Kwenye mpira kuna vipindi tofauti. Unaweza kutotendewa haki kama hivi, lakini unatakiwa unyanyuke na usonge mbele," alisema kocha huyo.



# Aguero pigo kwa Guardiola

**MANCHESTER,** England

MAMBO si shwari tena ndani ya Klabu ya Manchester City, ambapo nyota wake, Sergio Aguero anatarajia kuwa nje ya dimba kwa muda.

Ahuero alipata majeraha katika mchezo wao uliomalizika kwa sare ya bao 1-1 dhidi ya West Ham United mwishoni mwa wiki.

City imeshinda michezo miwili katika mechi tano za ufunguzi wa mwanzoni mwa ligi ikiwa inashika nafasi ya 12 kwa alama nane.

Sare hiyo iliifanya kuwa kwenye hali mbaya na hofu imezidi kuwa kubwa baada ya mfungaji wao bora wa muda wote kupata majeraha katika kipindi cha kwanza cha mchezo uliopita na yanaweza kumweka nje kwa muda mrefu zaidi.

Kocha wa kikosi hicho, Pep Guardiola alipoulizwa kuhusiana na suala hilo, alisema hajajua itachukua muda gani kupona.

"Alikuwa amepona kabisa kuanzia mchezo na Arsenal na huu, lakini anaonyesha kupata majeraha tofauti na hayo aliyowahi kupata hapo awali. Sijajua itamchukua muda gani. Nafikiri taarifa kamili itatoka baada ya kufanyiwa vipimo," alisema akinukuliwa na Sky Sport.

Hii si mara ya kwanza kwa Aguero kupata majeraha ndani ya mwaka huu. Juni mwaka huu alikumbana na jeraha la goti lililomweka nje kwa zaidi ya miezi minne, kabla ya kurejea tena mwezi huu na kucheza mechi ya kwanza dhidi ya Arsenal.

Pep amekuwa na mzimu wa majeraha unaokiandama kikosi chake tangu msimu uliopita akiwa na wachezaji wengi wa kikosi cha kwanza wana majeraha miongoni mwao ni kiungo wake tegemeo, Kevin De Bruyne, Aymeric Laporte, Fernandinho na Nathan Ake.

"Nilipenda kuwa napata ushindi katika michezo hii mitano hasa mchezo na West Ham, lakini imekuwa ni tofauti kwa kuwa wachezaji wangu wengi wamekumbana na majeraha na ratiba inaonekana kuwa ngumu," alisema.





# UNITED SASA KUINGIA VITANI KWA TRAORE

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inataka kuingia kwenye vita na Barcelona katika harakati za kuiwania saini ya winga wa Wolves, Adama Traore katika dirisha lijalo la majira ya joto.

Traore amekuwa ni miongoni mwa wachezaji ambao wanaonyesha kiwango kikubwa katika Ligi Kuu, England akisifika kwa uwezo wake mkubwa wa kuwa na kasi ya mashambulizi.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, kocha wa Man United, Ole Gunnar Solskjaer, amekuwa akiihusudu sana saini ya mwamba huyo kwa kuwa anaamini anaweza kuwa msaada kwenye timu yake baada ya dili la Sancho kushindikana.

Mkataba wa mchezaji huyo unatarajiwa kumalizika mwaka 2023 na Wolves inaripotiwa kuhitaji kiasi kisichopungua pauni milioni 70, ili kumuuza, Barcelona ilikuwa inaitamani sana saini yake katika dirisha lililopita, lakini dili hilo halikufanikiwa.

# *Mourinho akunwa na urafiki wa Kane, Son*

**LONDON,** England

JOSE Mourinho anaamini upatina wa Harry Kane na Son Heung-min umeimarika zaidi kwa sababu ya urafiki wao imara dimbani.

Tottenham walipata ushindi wa 1-0 dhidi ya Burnley Jumatatu shukrani kwa bao la dakika za majeruhi la Son, ambalo lilitengenezwa na Kane.

Ilikuwa ni mara ya tisa kwa wawili hao wa Spurs kutengenezeana bao msimu huu.

Na Mourinho anaamini urafiki wao ndio umekuwa nguzo kubwa ya wawili hao kufanya vizuri zaidi msimu huu.

"Walikuwa katika timu ambayo ni tofauti kabisa na timu ya msimu huu, lakini wanacheza pamoja kwa muda mrefu," alisema Mourinho, ambaye kikosi chake kipo nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi akiwaambia waandishi.

"Kwa uhakika kabisa urafiki wao ndani ya dimba ni mkubwa zaidi na ndio unaipa mafanikio makubwa zaidi Tottenham.

"Na hilo ni jambo la muhimu zaidi kwa timu kwa sababu wanaisaidia kupata mafanikio makubwa zaidi."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA ILIVYOMKATAA HAALAND CAMP NOU

●●● Nilipeleka jina lake, lakini niliambiwa hana uwezo wa kucheza hapa, yaani nilitengwa kwa...

**BARCELONA,** Hispania

MSHAURI wa zamani wa Barcelona, Ariedo Braida, amedai miamba hao wa LaLiga walikataa nafasi ya kumsajili Erling Haaland kabla ya nyota huyo wa Norway kung'ara, kwa sababu walimwona hafiti kucheza pale Camp Nou.

**Haaland haraka alichomoza kama mmoja wa mastraika bora duniani, aking'ara kule kwa mabingwa wa Austria, Salzburg kabla ya kujiunga na miamba ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Borussia Dortmund, Januari mwaka huu.**

Dogo huyo mwenye umri wa miaka 20, amefunga mabao 44 katika mechi za mashindano yote msimu wa 2019-20 - kati ya hayo 16 yakija katika mechi 18 za Salzburg kabla ya kutua Dortmund.

Haaland tayari ana mabao matano kwenye Bundesliga msimu huu, huku akifunga mabao saba katika mashindano yote.

Braida, ambaye aliondoka Barca mwaka 2019, alibainisha kwamba miamba hao wa Catalunya hawakuwa na mpango na Haaland wakati akicheza pale Molde.

"Nilikuwa mfuatiliaji wa wachezaji na niliandika majina ya wachezaji kama Haaland kutoka Borussia Dortmund, wakati akiwa bado anacheza kule Norway," alisema Braida akiliambia gazeti la Marca.

"Lakini klabu iliniambia mimi, hapana, kwamba hana uwezo wa kucheza Barcelona, pia nilishauri wachezaji kutoka Italia, kama (Nicolo) Barella, ambaye kwa sasa anacheza Inter Milan, au (Nicolo) Zaniolo, ambaye anacheza AS Roma.

"Lakini kama huna majukumu ya kufanya haya inapelekwa kwa watu wengine na ndivyo nilivyofanyiwa mimi. Yaani nilitengwa kwa ushauri wangu."

Haaland anatarajia kucheza mechi yake ya 10 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhiai ya Zenit leo, Jumatano.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway tayari ana nafasi ya kuwa mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote wa kikosi hicho kuelekea mechi yake ya 10 katika mashindano hayo, huku Haaland akiwa kafunga mabao 11 katika mechi tisa hadi sasa.

## ZISIKUPITE

### MUSTAFI KUONDOKA ARSENAL

MLINZI wa Ujerumani, Shkodran Mustafi, mwenye umri wa miaka 28, amekataa ofa ya mkataba mpya Arsenal na ameitaarifu klabu hiyo kwamba ana mpango wa kuondoka mkataba wake wa sasa utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Football London)***

### LAMPARD, RUDIGER WATETA

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, yuko tayari kumjumuisha Antonio Rudiger kwenye mipango yake ya kikosi cha kwanza, baada ya mazungumzo ya kina na mlinzi huyo wa kati wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 27, ambaye amekuwa akihusishwa na timu za Tottenham na Paris St-Germain. ***(Mail)***

### PALACE, ANDROS KUMALIZANA

KLABU ya Crystal Palace imeanza mazungumzo na winga wa England, Andros Townsend mwenye umri wa miaka 29, kuhusu mkataba mpya baada ya kufanikiwa kuzima mipango ya West Brom iliyokuwa inamtaka kipindi cha majira ya joto. ***(Football Insider)***

### ROSE, SPURS KIMEELEWEKA

KLABU ya Tottenham Hotspur ina matumaini ya kufikia makubaliano ya kusitisha mkataba na mlinzi wa kushoto raia wa Uingereza, Danny Rose, 30, anatarajia kulipwa zaidi ya pauni 2.5 ya thamani ya mkataba wake uliobaki, ambao unamalizika mwakani. ***(Football Insider)***

### LIVERPOOL YAMPOTEZEA KABAK

LIVERPOOL haina mpango wa kumsajili mlinzi wa Schalke, Ozan Kabak, mwenye umri wa miaka 20 raia wa Uturuki. ***(Liverpool Echo)***

### WACHEZAJI WAMKUBALI MOYES

WACHEZAJI wa West Ham wanamuunga mkono kocha wao, David Moyes na wanataka aongezewe mkataba mpya. ***(Mail)***

### UMTITI AIKATAA ARSENAL

MLIZI wa kati wa Barcelona na Ufaransa, Samuel Umtiti mwenye umri wa miaka 26, amekataa mazungumzo ya kujiunga na Arsenal. ***(Canal+, via Football London)***

### RONALDO ACHUNGUZWA ITALIA

WAZIRI wa michezo wa Italia, Vincenzo Spadafora, amesema mshambuliaji wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo, 35, anachunguzwa kwa kurudi nchini humo wakati akiwa na virusi vya corona. ***(Star)***

### LASNBURY AIKATALIA VILLA

KIUNGO wa Uingereza, Henri Lansbury, 30, amekataa ofa kutoka Aston Villa ya kumaliza mkataba wake na klabu hiyo. ***(The Athletic, via Birmingham Mail)***

### GUARDIOLA ATOA SIRI CITY

PEP Guardiola amesisitiza Manchester City ilifikiria kumsajili straika kipindi cha majira ya joto, lakini haikuweza kumpata wanayemhitaji. ***(Manchester Evening News)***

### ESSIEN AMPA MBINU LAMPARD

KIUNGO wa zamani wa Chelsea, Michael Essien, amemtaka Frank Lampard kutafuta mfumo mzuri pale Stamford Bridge baada ya kuwa na mwanzo mgumu. ***(Goal.com)***

## Katwila ataka subira Ihefu FC

**Na Shufaa Lyimo**

HUKU akipata alama moja katika mechi mbili tangu aanze kuinoa Ihefu FC, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zuberi Katwila, amewaomba mashabiki wao kuvutia subira wakati huu akijitahidi kurekebisha makosa yaliyopo katika kikosi hicho.

Katwila alianza kuinoa Ihefu katika mchezo wa kwanza Ligi Kuu dhidi ya Azam FC, ambao waliangukia kichapo cha mabao 2-0 kabla ya kutoka sare tasa dhidi ya Namungo FC, mechi zote zikipigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila alisema mapungufu aliyoyakuta ni vigumu kuisha haraka, hasa kutokana na kutokuwa na muda wa kujiandaa na msimu, hivyo kulazimika kutumia mechi hizo za ligi kadri zinavyoendelea.

"Mpaka sasa nina kazi moja ya kuhangaika na makosa ambayo niliyakuta, hayawezi kuisha haraka ninaomba mashabiki wetu wavute subira mambo mazuri yanakuja," alisema Katwila.

Alisema anafurahishwa na ushirikiano anaoendelea kupewa na viongozi pamoja na wachezaji kitu ambacho kinampa matumaini ya kupata mafanikio.

Alisema kwa sasa anaelekeza nguvu zake kujiandaa na mchezo ujao watakaokutana nao dhidi ya Mbeya City Novemba 2, mwaka huu.

## JKU yapania ubingwa Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya JKU imesema mkakati wake msimu huu ni kuhakikisha inafanya vizuri ili kuunyakuwa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu wa 2020/2021.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Sadu Ujudi, alisema timu yake imefanya usajili mzuri ambao utatoa ushindani katika ligi hiyo ambayo inatabiriwa kuwa ngumu kutokana na uchache wa timu zinazoshiriki msimu huu.

Alisema katika kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri kwenye michezo yake, tayari imecheza mechi sita za kirafiki na yote kupata matokeo mazuri huku kocha aridhika na viwango vya wachezaji wake.

Aidha, alisema kikosi ambacho kwa sasa kimesimamisha mazoezi ili kupisha uchaguzi mkuu, kimesajili wachezaji watano kutoka madaraja tofauti ili kutimiza lengo lake la kuunyakuwa ubingwa wa Zanzibar kwa msimu huu.

Ligi Kuu Zanzibar inatarajiwa kuanza rasmi Novemba 14, mwaka huu.

# AZAM YATOA SABABU KIPIGO KWA MTIBWA

**Na Saada Akida,** MOROGORO

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amefichua kilichopo nyuma ya kipigo chao dhidi ya Mtibwa Sugar kuwa ni kuzidiwa katika idara ya kiungo pamoja na mabadiliko ya mfumo ambao waliotumia katika mechi hiyo tofauti na michezo iliyopita ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Ikiwa ugenini katika Uwanja wa Jamhuri mjini Mororogo juzi, Azam ilipoteza mechi yake ya kwanza msimu huu kwa kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, shukrani zikimwendea Jafar Kibaya aliyeipa ushindi katika dakika ya 61 kwa shuti kali la mbali ambalo lilimshinda kipa David Kisu.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Vivier alisema Mtibwa walikuwa vizuri katika idara ya kiungo, jambo ambalo lilichangia kupata ushindi huo, lakini mfumo waliotumia hakuwa rafiki kwao katika mechi hiyo.

Alisema hawakukiona kile ambacho walikihitaji katika mfumo huo, licha ya kupata nafasi nzuri na kushindwa kuzitumia kupata ushindi.

"Ni kweli kuchoka ni sehemu ya mechi, maana tumepiga pasi nyingi kisha zikaishia njiani, lazima uchoke kutokana na kutumia nguvu nyingi kwa kukaba pia.

"Wachezaji wamefanya kazi nzuri mwisho wa siku matokeo hayakuwa upande wetu. Tumepoteza mchezo wetu wa kwanza kwa msimu huu," alisema Vivier.

Aidha, alisema kutokuwapo kwa nyota wao wawili, Obrey Chirwa na Salum Abubakar "Sure Boy" hakukuiathiri timu hiyo, ila sababu kubwa ni bahati kutokuwa upande wao.

Lakini kwa upande wa Kaimu Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Vincent Barnaba, alisema licha ya kupata ushindi wa mechi mbili mfululizo tangu kuachia ngazi kwa Kocha Mkuu, Zuberi Katwila, bado ana safari ndefu ya kuipa mafanikio.

Barbana alisema kushinda mechi mbili mfululizo hakutamfanya kujiona bora zaidi, bali anaamini bado safari ni ndefu kufikia malengo ya kufanya vizuri na kutoishia kuwa washiriki katika ligi hiyo.

"Bado nina uwoga, si kazi rahisi kukaa miaka mitano na kuaminiwa, kusimamia timu ni ngumu, ukiangalia waliopita walikaa miaka zaidi yangu wakiwa wasaidizi akiwamo Salim Mayanga aliyekuwa kocha msaidizi kwa miaka 10, hata kwa Mecky Maxime na Katwila walikaa miaka saba.

"Kwangu ni muda mfupi sana ukizingatia na waliopota mbele yangu, hivyo kikubwa ni kuzungumza na wachezaji wapambane tupate matokeo mazuri katika mechi zetu zote za ligi hiyo," alisema Barnaba.

**UWEZO...**



Wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Kiislam ya Al- Faruku, wakionyesha uwezo wao wa michezo mbalimbali wakati wa mahafali ya nane ya kumaliza elimu ya msingi na madarasa ya awali yaliyofanyika shuleni hapo, Tabata jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mkwasa aanika siri Ruvu Shooting kuichapa Simba

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwasa, amesema waliingia na mkakati wa kuwamaliza Simba kipindi cha kwanza, jambo ambalo lilifanikiwa na kupata matokeo kwenye mechi hiyo ya juzi iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya mechi hiyo ambayo timu yake iliichapa Simba bao 1-0 shukrani zikimwendea Fully Maganga aliyepeleka msiba Msimbazi, dakika ya 35 baada ya timu yake kufanya shambulizi la kushtukiza, Mkwasa alisema waliisoma Simba na kugundua kuwa wanakuwa wazuri mno kipindi cha kwanza, hivyo ukiwabana na kushindwa kupata bao, basi wanakuwa hawana cha zaidi kipindi cha pili.

"Unajua ni rahisi kumsoma mkubwa, lakini si rahisi mkubwa kumsoma mdogo. Sisi tuliwasoma Simba na tukaingia na mkakati wetu wa kuimaliza kipindi cha kwanza na kweli tulipata bao tukawa tumekaa sehemu nzuri," alisema Mkwasa ambaye ni mchezaji na kocha wa zamani wa Yanga.

Alisema katika mechi hiyo waligawana vipindi, wao wakicheza kipindi cha kwanza na Simba wakikitawala kipindi cha pili, huku akikiri ulikuwa ni mpira wa kutumia nguvu zaidi.

"Ulikuwa ni mpira wa nguvu, Simba waliingia kipindi cha pili kwa nguvu na kusukuma zaidi mashambulizi na naweza kusema kipindi cha pili sasa walicheza kama timu mpaka wakapata penalti, lakini wakakosa," alisema.

Rekodi zinaonyesha kuwa katika mechi za Ligi Kuu msimu huu, Simba inaonekana kupata mabao zaidi kipindi cha kwanza kuliko cha pili.

Baada ya kipigo hicho, Simba inakuwa kwenye nafasi ya nne ikiwa imebaki na pointi zake 13, Azam pamoja na kufungwa bao 1-0 na Mtibwa Sugar, badi ipo kileleni na pointi 21, Yanga ikishika nafasi ya pili na alama zake 19, huku Biashara United ikiwa nafasi ya tatu na pointi 16 kibindoni.

# Michezo

Jumatano Oktoba 28, 2020
Nipashe



Barca ilivyomkataa Haaland Camp Nou UKURASA 22

MILIKI...



Mshambuliaji wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic, akimiliki mpira dhidi ya mabeki wa AS Roma wakati wa mechi ya Ligi Kuu Italia, Serie A iliyopigwa Uwanja wa Giuseppe Meazza juzi na timu hizo kutoka sare ya mabao 3-3. Kwa mabao hayo sasa yanamfanya Ibrahimovic kukaa kileleni mwa orodha ya wafungaji katika ligi hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# KAZE APATA DAWA YA BIASHARA UNITED

## ●●● Lakini akiri Ligi Kuu Bara ni ngumu, Sarpong aungana naye huku akifunguka mabao sasa...

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU kikosi chake kikiendelea kujifua jijini Mwanza kabla ya kuifuata Biashara United, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema mechi iliyopita dhidi ya KMC FC iliyopigwa katika Uwanja wa CCM Kirumba, imempa mbinu ya nanma ya kukabiliana na wapinzani wao wakiwa viwanja vya ugenini.

**Katika mechi hiyo ambayo Yanga ilishinda mabao 2-1, safu yao ya ushambuliaji ilikuwa chini ya washambuliaji wawili, Michael Sarpong pamoja na Waziri Junior ambaye aliifungia timu yake bao la ushindi baada ya Tuisila Kisinda kusawazisha lile la awali lililofungwa na Hassan Kabunda dakika ya 18.**

Kaze alisema Waziri Junior amempa suluhisho la namna ya kukabiliana na mechi za ugenini hususan wanapokuwa nje ya Dar es Salam, na kwamba sasa atakuwa akichezesha washambuliaji wawili badala ya mmoja kama ambavyo alifanya dhidi ya Polisi Tanzania katika Uwanja wa Uhuru.

Alisema amegundu Ligi Kuu Bara ni ngumu tofauti na alivyokuwa akiichukulia, lakini kuchezesha washambuliaji wawili na kucheza pasi ndefu na mpira wa kasi akiwa ugenini ni mbinu ambazo zinaweza kuendelea kuwapa matokeo.

Alisema hiyo inatokana na wapinzani wao kucheza mipira mirefu, hivyo inakuwa vigumu kucheza na straika mmoja, jambo ambalo atakuwa akitumia mastraika wawili.

"Waziri Junior alinipa 'options' (mbadala) wa kucheza na straika wawili, kwa viwanja kama hivi unapaswa kuanza na washambuliaji wawili kulingana na namna wapinzani wanavyocheza," alisema Kaze, ambaye ni raia wa Burundi.

Wakati Kaze akieleza hayo, straika namba moja wa timu hiyo, Sarpong naye amekiri Ligi Kuu Bara ni ngumu lakini anaamini wakati wake wa kuifungia mabao timu hiyo sasa umewadia.

Licha ya kuanza mechi zote za Yanga, Sarpong amefunga bao moja tu hadi sasa, ambalo alilipata wakati wakitoka sare ya 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons kwenye mechi ya ufunguzi wa ligi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Mkapa. Sarpong ambaye msimu uliopita alichezea Rayon Sports ya Ligi Kuu Rwanda, alisema: "Mambo yanabadilika kadiri muda unavyokwenda, kawaida yangu huwa sina woga nikiwa uwanjani kwa sababu napenda kuipigania timu kupata matokeo bila ya kujali nimefunga mimi ama la.

"Ninachokiangalia kwa sasa ni kufunga, naamini sasa muda umewadia wa kufanya hivyo, nimeshajua ugumu wa mabeki ulipo na namna ya kukabiliana nao katika kuhakikisha nafunga, kwa kuwa hilo ndilo jambo kubwa katika akili yangu," alisema straika huyo raia wa Ghana.

Yanga ambayo ni timu pekee hadi sasa Ligi Kuu Bara haijapoteza mechi yoyote, ina pointi 19 katika nafasi ya pili, ikiwa ni alama mbili nyuma ya vinara Azam FC ambao juzi walionja kipigo cha kwanza wakiwa ugenini dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

## Meneja Simba atimuliwa, Kocha Sven aomba radhi

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, akiwaomba radhi mashabiki wa timu hiyo kutokana na kupoteza mechi mbili za Ligi Kuu mfululizo, uongozi wa klabu hiyo umemtimua Meneja wao, Patrick Rweyemamu.

Simba juzi ilikubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Ruvu Shooting katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam ikiwa ni siku tano baada ya kuangukia pua kwa kichapo kama hicho kutoka kwa Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga.

Lakini Sven alisema kupoteza mechi hiyo ya juzi, si suala la wachezaji wake kutokuwa fiti na kama ingekuwa hivyo, wasingeweza kushambulia kwa kasi kipindi cha pili kama ambavyo walifanya.

"Kupoteza mechi mbili mfululizo si jambo zuri, mashabiki watusamehe wasivunjike moyo, kuna mambo ambayo siwezi kuyaongea kwa vyombo vya habari tutakwenda kuyashughulikia kikosini.

"Sikutarajia kuona tunapoteza mchezo mwingine tena, lakini ndio mpira ulivyo muda mwingine una matokeo ya kuumiza, tuendelee kuwa na umoja benchi la ufundi linafanyia kazi upungufu uliopo," alisema Sven.

Kwa upande wa Meneja wa Simba, Rweyemamu alipoulizwa na Nipashe, alikiri kupokea barua ya kuachishwa kazi kutoka kwa uongozi wa klabu hiyo.

"Ni kweli baada ya mechi ya jana (juzi) dhidi ya Ruvu Shooting, nilipokea barua kutoka kwa uongozi ya kuachishwa kazi," alisema Rweyemamu bila kufafanua zaidi.

Hata hivyo, chanzo chetu ndani ya klabu hiyo kilieleza sababu ya meneja huyo kuachishwa kazi ni kutokana na mambo kutokwenda sawa kambini.

Simba inajiandaa kukutana na Mwadui FC Jumamosi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam na baada ya hapo itabakisha mchezo mmoja dhidi ya Kagera Sugar kabla ya kukutana na watani zao, Yanga Novemba 7, mwaka huu katika dimba la Mkapa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >